JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA FEDHA

# MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25

NOVEMBA, 2023



# MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25

**YALIYOMO**


ORODHA YA VIFUPISHO ........ ii

MUHTASARI ........ iii

1. MUHTASARI WA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI ........ 1
1.1 Mwenendo wa Uchumi ........ 1
1.2 Deni la Serikali ........ 4
2. VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25 ........ 5
2.1 Vipaumbele ........ 5
2.2 Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla ........ 7
2.3 Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 ........ 7
3. USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI ........ 20
3.1 Vihatarishi vya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ........ 20
3.2 Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi ........ 23
4. MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25 26
4.1 Maandalizi ya Mpango na Bajeti ........ 26
4.2 Maelekezo ya Jumla ya Uandaaji wa Mpango na Bajeti ........ 30
4.3 Maelekezo Mahsusi kwa Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma ........ 38
4.4 Maelekezo kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ........ 39
4.5 Masuala Mengine Muhimu ya Kuzingatiwa wakati wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti ........ 43
4.6 Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ........ 49

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AU | African Union |
| CBMS | Centralized Budget and Management System |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| DCF | Development Co-operation Framework |
| EAC | East African Community |
| EFD | Electornic Fiscal Device |
| EU | European Union |
| GBS | General Budget Support |
| GFS | Government Finance Statistics |
| GoT HOMIS | Government of Tanzania Health Operation Management |
| HCMIS | Human Capital Management Information System |
| JKT | Jeshi la Kujenga Taifa |
| MTDS | Medium Term Debt Strategy |
| MTEF | Medium Term Expenditure Framework |
| MW | Megawatts |
| NeST | National e-Procurement System of Tanzania |
| NPMIS | National Project Management Information System |
| OR-MUUUB | Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PlanRep | Planning and Reporting Database |
| SMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| SMZ | Serikali ya Muungano wa Zanzibar |
| TARURA | Tanzania Rural and Urban Roads Agency |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UVIKO – 19 | Ugonjwa wa Virusi vya Korona |
| VAT | Value Added Tax |
| VVU | Virusi Vya Ukimwi |

## KAULI YA KATIBU MKUU HAZINA NA MLIPAJI MKUU WA SERIKALI KUHUSU MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 umeandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake za mwaka 2015. Mwongozo umeainisha masuala ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wote wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma wakati wa maandalizi, utekelezaji, ufuatiliaji tathmini na utoaji wa taarifa za mpango na bajeti.

Maafisa Masuuli mnasisitizwa kuandaa bajeti zenu za mwaka 2024/25 kwa umakini mkubwa kwa kuzingatia wigo wa ukomo wa bajeti utakaotolewa kwa kila fungu, maelekezo ya Mwongozo na vipaumbele vya taifa vya mwaka 2024/25. Aidha, ili kuwianisha mapato na matumizi, mnasisitizwa kutenga bajeti kwenye maeneo ya vipaumbele vya kisekta na majukumu ya msingi ya Taasisi zenu kwa mujibu wa "Instrument", na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali.

Katika kusimamia dhana ya uwajibikaji na uwazi katika utendaji kazi, mnatakiwa kuhakikisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kinafuatilia uzingatiwaji wa Sheria ya Bajeti kuhusu utendaji wa Kamati ya Bajeti kwa lengo la kupitia na kujadili taarifa za ufuatiliaji, tathmini na utekelezaji kila robo mwaka ili kuleta uwajibikaji. Aidha, mnaelekezwa kudhibiti uzalishaji wa madeni, kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kudhibiti na Kuzuia Malimbikizo ya Madeni ulioboreshwa wa mwaka 2022 na maelekezo ya *Treasury Circular No. 2 of 2022/23 on Government Domestic Expenditure Arrears and Other Outstanding Obligations.*

Ni matarajio yangu kuwa mtazingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti, Sura 439; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na Miongozo ya Serikali katika kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya Serikali kwa tija na ufanisi ili kutoa huduma bora kwa wananchi. Utekelezaji wa Mipango na Bajeti zenu kwa tija na ufanisi utaimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma; utawala bora na utawala wa sheria; kutoa fursa za ajira; kuongeza ushiriki wa wadau katika uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango na Bajeti na hatimaye kuchochea ukuaji wa uchumi na kuongeza upatikanaji wa huduma za jamii kwa wote

Ninawatakia utekelezaji mwema.

Mwamba

Dkt. Natu E. Mwamba
**KATIBU MKUU NA**
**MLIPAJI MKUU WA SERIKALI**

**MUHTASARI**

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali umeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Mwongozo wa mwaka 2024/25 ni wa nne (4) katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Pamoja na mambo mengine, maandalizi ya Mwongozo huu yamezingatia: Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); maelekezo mahsusi ya Serikali; na Agenda ya Afrika 2063. Lengo la Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ni kutoa maelekezo kuhusu maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2024/25 kwa Maafisa Masuuli wote kuandaa mipango yao na bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa na kisekta pamoja na Sheria za Nchi, Kanuni, Nyaraka na Miongozo mbalimbali ya Kisekta na Serikali kwa ujumla.


Pamoja na umuhimu na ulazima wa kuzingatia maeneo ya kipaumbele ya Kisekta na Kitaifa katika maandalizi ya mipango na bajeti za mafungu maeneo mengine ya kuzingatia ni: maelekezo ya jumla kuhusu uandaaji wa Mpango na Bajeti; Maelekezo mahususi kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma; Usimamizi wa vihatarishi vya Mpango na Bajeti ikijumuisha uainishaji, mikakati na ufuatiliaji na tathmini; masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi; masuala ya Muungano na mashirikiano ya kikanda na Kimataifa. Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni: Muhtasari wa mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi; vipaumbele vya mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25; usimamizi wa vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti; na maelekezo ya maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka 2024/25. Aidha, Mwongozo huu unapaswa kusomwa pamoja na viambatisho vyake vyote.

Utekelezaji wa maelekezo ya Mwongozo huu utachangia: Kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha za umma; kuendelea kuhimili athari zitokanazo na

kudorora kwa uchumi wa dunia na kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma katika soko la dunia; kuondoa uhamisho wa bajeti usio wa lazima; kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara; kutoa fursa za ajira; kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili; kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini; kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii kwa wote na uwepo wa amani, usalama, utawala bora na utawala wa sheria, umoja na utulivu nchini. Hivyo, Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kuzingatia maelekezo ya mwongozo huu kwa ukamilifu.



# 1 MUHTASARI WA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI



# 1

# MUHTASARI WA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI

# 1. MUHTASARI WA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI

Sehemu hii inaelezea mwenendo wa hali ya uchumi wa dunia, kikanda na Tanzania kwa mwaka 2022 na mwelekeo wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2023 hadi mwaka 2024.

## 1.1 Mwenendo wa Uchumi

### 1.1.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Kikanda

1. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imepungua kutokana na athari za janga la UVIKO-19, vita kati ya Urusi na Ukraine pamoja na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa toleo la Oktoba 2023, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.3 mwaka 2021. Mwaka 2023, uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.0 na asilimia 2.9 mwaka 2024. Katika nchi zilizoendelea uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.6 mwaka 2021. Kwa upande wa nchi zinazoibukia na zinazoendelea, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2021. Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, uchumi ulishuka kutoka asilimia 4.7 mwaka 2021 hadi asilimia 4.0 mwaka 2022.

### 1.1.2 Ukuaji wa Uchumi wa Tanzania

2. Pamoja na changamoto zilizojitokeza na kuathiri uchumi wa dunia, uchumi wa Tanzania uliendelea kuimarika kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ikiwemo utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine; na utoaji wa ruzuku ya mbolea na mafuta ya petroli. Uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 4.7 kwa mwaka 2022, na unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.2 mwaka 2023 na asilimia 5.8 mwaka 2024. Pamoja na mambo mengine, ukuaji wa uchumi ni matokeo ya uwekezaji wa kimkakati wa Serikali katika miundombinu ya nishati, huduma za kijamii na usafirishaji, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini na

shughuli za utalii. Shughuli za kiuchumi zilizochangia kwa sehemu kubwa katika ukuaji huo ni kilimo, ujenzi na uchimbaji wa madini.

### 1.1.3 Mfumuko wa Bei Nchini

3. Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.6 mwaka 2022/23, kiwango ambacho kipo ndani ya lengo la nchi na mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC). Aidha, mfumuko wa bei kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2023 ulikuwa wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 4.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 3.0 – 7.0 ambalo linaendana na viwango vya kikanda kutokana na matarajio ya hali nzuri ya hewa, utulivu wa bei za bidhaa katika soko la dunia pamoja na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti.

### 1.1.4 Ujazi wa Fedha na Mikopo

4. Mwaka 2022/23, Benki Kuu ilitekeleza sera ya fedha iliyolenga kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi kwenye uchumi ili kukabiliana na shinikizo la ongezeko la mfumuko wa bei linalotokana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine, athari za janga la UVIKO-19 na mabadiliko ya tabianchi bila kuathiri kasi ya ukuaji wa uchumi. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 13.7, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 12.2 katika mwaka 2021/22 na lengo la ukuaji wa asilimia 10.3 kwa mwaka 2022/23. Aidha, wastani wa fedha taslimu ulikua kwa asilimia 12.8 ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 11.4. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 22.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.9 mwaka 2021/22 na lengo la ukuaji wa asilimia 10.7.

### 1.1.5 Viwango vya Riba

5. Mwaka 2022/23, riba ya jumla katika soko la fedha baina ya mabenki iliendelea kuwa tulivu kwa wastani wa asilimia 3.55 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.22 kwa mwaka 2021/22. Aidha, riba ya jumla ya dhamana za

muda mfupi za Serikali zilifikia wastani wa asilimia 5.73. Viwango vya riba zinazotozwa na benki kwa mikopo vilikuwa wastani wa asilimia 16.04 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.41 mwaka 2021/22. Aidha, wastani wa viwango vya jumla vya riba za amana ulifikia asilimia 8.01 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.18 mwaka 2021/22.

#### 1.1.6 Viwango vya Ubadilishaji Fedha

6. Katika kipindi cha mwaka 2022/23, thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilipungua kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni kwenye uchumi kufuatia ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia na kupungua kwa fedha za kigeni zinazoingia nchini kutokana na kupanda kwa riba za benki kuu katika nchi zilizoendelea. Dola moja ya Marekani katika soko la jumla ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,321.69 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi 2,309.50 mwaka 2021/22. Aidha, katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,428.26 ikilinganishwa na shilingi 2,316.73 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

#### 1.1.7 Sekta ya Nje

7. Sekta ya nje imeendelea kukabiliwa na changamoto zinazotokana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine, na UVIKO-19. Hali hii imesababisha kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi wa bidhaa na huduma duniani na hivyo kusababisha kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia. Kutokana na changamoto hizi, urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje ulifikia nakisi ya dola za Marekani milioni 4,860.1 mwaka 2022/23.

8. Akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani bilioni 5.45, mwishoni mwa mwezi Juni 2023, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.9. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi mahitaji ya miezi 4.0 na zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### 1.1.8 Sekta ya Benki na Huduma za Fedha

9. Sekta ya benki imeendelea kuimarika na kutengeneza faida ikiwa na viwango vya kutosha vya mitaji na ukwasi. Ubora wa rasilimali za benki umeendelea kuimarika ambapo mikopo chechefu ilipungua hadi wastani wa asilimia 5.3 Juni 2023 kutoka asilimia 7.8 Juni 2022. Hali hii ilichangiwa zaidi na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kwa kuboresha mazingira ya kufanya biashara na usimamizi thabiti wa benki. Kwa mujibu wa utafiti wa huduma za fedha wa mwaka 2023 (Tanzania Finscope Survey, 2023) asilimia ya watu wazima wanaotumia huduma za fedha imeongezeka kutoka asilimia 65 mwaka 2017 hadi asilimia 76 mwaka 2023. Aidha, utafiti huo ulibainisha kuwa watanzania wengi wanazifikia na kutumia huduma za fedha kupitia simu za mkononi.

## 1.2 Deni la Serikali

10. Hadi Juni 2023, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 82,137.9. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi bilioni 28,926.37 na deni la nje ni shilingi bilioni 53,211.53. Aidha, tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba, 2022 inaonesha kuwa viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda wa kati na mrefu. Mwaka 2022/23, tathmini ya uwezo wa nchi kukopesheka (Credit Rating) ilikamilika ambapo kampuni za Moody's Investors Service Ltd na Fitch Rating Services Ltd zilichapisha matokeo ya daraja B2+ na B+ mtawalia. Alama hizo zinabainisha kuwa mwelekeo wa hali ya uchumi, usimamizi wa deni, uwekezaji na hali ya kisiasa nchini ni ya kuridhisha.

Taarifa ya kina kuhusu mwenendo wa uchumi wa dunia, kikanda na Tanzania inapatikana katika **Kiambatisho Na. 1A.**



# 2 VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

# 2

# VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

## 2. VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

Sehemu hii inaelezea vipaumbele vya mpango na bajeti ya Serikali; shabaha na misingi ya uchumi jumla; makadirio ya mapato na matumizi; na mikakati ya kuongeza mapato na usimamizi wa matumizi kwa mwaka 2024/25.

### 2.1 Vipaumbele

11. Bajeti ya Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika maeneo yaliyoainishwa kwenye mipango ya maendeleo ya muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika muda wa kati, Serikali itatekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambavyo vimegawanyika katika maeneo matano: Kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu. Aidha, eneo la utekelezaji wa miradi ya kielelezo limepewa kipaumbele cha kipekee kutokana na kuwa na matokeo makubwa na mtambuka kwenye uchumi na jamii (multiplier effects). Hivyo, vipaumbele kwa mwaka 2024/25 vitazingatia maeneo yafuatayo:

i. **Kuendelea na Utekelezaji wa miradi ya Kielelezo:** Miradi itakayopewa kipaumbele katika eneo hili ni ambayo utekelezaji wake unaendelea. Miradi hiyo ni: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania; Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge); Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); ujenzi wa madaraja makubwa na barabara za Juu (Interchange) ikiwemo Daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza); ujenzi wa Bandari ya Uvuvi (Kilwa) na ununuzi wa meli za uvuvi; na ujenzi wa kiwanda cha Sukari Mkulazi. Aidha, miradi mingine ni: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358); Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Rumakali (MW 222); na Mradi wa Magadisoda - Engaruka. Katika kutekeleza miradi hii kwa ufanisi Serikali itaendelea

kutekeleza programu ya kuongeza rasilimali watu wenye ujuzi adimu na maalumu kwa maendeleo ya viwanda na ustawi wa jamii.

ii. **Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi:** Eneo hili limejielekeza katika utekelezaji wa miradi ambayo inalenga kuboresha mazingira wezeshi ya uwekezaji, mapinduzi ya TEHAMA na kuimarisha miundombinu na mifumo ya kitaasisi. Miradi itakayotekelezwa itajumuisha ujenzi wa miundombinu ya reli, barabara, madaraja, TEHAMA, nishati, bandari na viwanja vya ndege.

iii. **Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma:** Eneo hili linajikita katika uimarishaji wa miundombinu na mazingira wezeshi ya uzalishaji viwandani ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, na uvuvi pamoja na madini, vito vya thamani na gesi asilia.

iv. **Kukuza Biashara na Uwekezaji:** katika eneo hili, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara na kukuza uwekezaji, kukuza uwezeshaji wananchi kiuchumi, kukuza sekta binafsi, huduma za biashara na masoko pamoja na mahusiano ya kidiplomasia ya uchumi na nchi za nje ili kuchochea uzalishaji wa bidhaa na kukuza biashara ndani na nje ya nchi.

v. **Kuchochea Maendeleo ya Watu:** Eneo hili linajikita katika utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali inayolenga kuboresha maisha ya watu hususan utekelezaji wa miradi na programu katika sekta za kijamii. Miradi hiyo inajumuisha: elimu na mafunzo ya ujuzi; afya, ustawi na maendeleo ya jamii; hifadhi na kinga ya jamii; huduma za maji na usafi wa mazingira; mipango miji, nyumba na maendeleo ya makazi; na hifadhi ya mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## 2.2 Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla

### 2.2.1 Shabaha za Uchumi Jumla

12. Kutokana na uchambuzi na maoteo yaliyofanyika, Pato Halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.2 mwaka 2023 na kuongezeka hadi asilimia 5.8 mwaka 2024; mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 hadi 7.0 katika kipindi cha muda wa kati; mapato ya kodi kufikia asilimia 12.4 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2024/25 kutoka uwiano halisi wa asilimia 11.9 uliofikiwa mwaka 2022/23; nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 2.2 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 2.7 ya mwaka 2023/24; kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na kuimarika kwa viashiria vya ustawi wa jamii.

### 2.2.2 Misingi ya Uchumi Jumla

13. Misingi iliyotumika katika kuandaa shabaha za uchumi jumla ni pamoja na: kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara; kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko, mafuriko); kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini; na uwepo wa amani, usalama, utawala bora na utawala wa sheria, umoja, utulivu wa ndani na nchi jirani.

## 2.3 Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25

### 2.3.1 Mapato


14. Katika mwaka 2024/25, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 47,424.9. Makadirio ya mapato yamezingatia vigezo mbalimbali ikiwemo mwenendo halisi wa ukusanyaji wa mapato; viashiria vya uchumi jumla; na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika

kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato. Aidha, kwa upande wa matumizi, makadirio yamezingatia mahitaji halisi ya ugharamiaji wa deni la Serikali, mishahara ya watumishi pamoja na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati inayoendelea.

#### 2.3.1.1 Mapato ya Ndani

15. Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 34,436.2 mwaka 2024/25 (**Kielelezo Na. 2.1**). Katika kipindi cha muda wa kati, mapato yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.5 na kufikia shilingi bilioni 38,957.0 mwaka 2026/27. Mchango wa mapato ya ndani katika bajeti unakadiriwa kuwa asilimia 72.6 mwaka 2024/25 na kuendelea kuongezeka hadi asilimia 75.8 mwaka 2026/27.

**Kielelezo Na. 2.1: Mchanganuo wa Mapato ya Ndani katika Muda wa Kati (Shilingi Bilioni)**





**Mchanganuo wa Mapato ya Ndani**

16. Katika mwaka 2024/25, mapato (kodi na yasiyo ya kodi) yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 29,520.7. Katika muda wa kati, mapato yanayokusanywa na TRA


yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.4 na kufikia shilingi bilioni 33,126.8 mwaka 2026/27. Uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa ni wastani wa asilimia 12.4 katika kipindi cha muda wa kati. Mchanganuo wa mapato yanayokusanywa na TRA ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 2.2.**

**Kielelezo Na. 2.2: Mchanganuo wa Mapato Yanayokadiriwa Kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika Muda wa Kati (Shilingi Bilioni)**




17. Mwaka 2024/25 mapato yasiyo ya kodi (Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa) yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 4,915.5. Kati ya makadirio hayo, shilingi bilioni 2,442.8 inatarajiwa kukusanywa na Wizara na Idara zinazojitegemea, shilingi bilioni 1,157.2 inatarajiwa kukusanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina, na shilingi bilioni 1,315.5 inatarajiwa kukusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika muda wa kati, mapato yasiyo ya kodi yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.8 na kufikia shilingi bilioni 5,830.2 mwaka 2026/27. Mchanganuo wa mapato yasiyo ya kodi ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 2.3**.

**Kielelezo Na 2.3: Mchanganuo wa Mapato Yasiyo ya Kodi katika Muda wa Kati (Shilingi Bilioni)**




### 2.3.2 Hatua na Mikakati ya Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

**Hatua**

i. Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini katika sekta za huduma na uzalishaji ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi;
ii. Kuongeza wigo wa walipakodi kwa kutambua na kusajili biashara zisizo rasmi na zinazoendeshwa kidigitali;
iii. Kuimarisha na kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato ya ndani;
iv. Kudhibiti misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja (1) ya Pato la Taifa; na
v. Kuendelea kuboresha utendaji wa mashirika ya umma ili kuongeza mchango wake katika mapato.

**Mikakati**

i. Kutanua wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuhakikisha vyanzo hivyo vinaakisi misingi ya ukusanyaji mapato;

ii. Kuendelea kufanya tathmini ya majukumu na utendaji wa taasisi na mashirika ya umma kwa lengo la kuongeza ufanisi na mapato ya Serikali;
iii. Kutekeleza Mkakati wa Uwajibikaji wa Ulipaji Kodi ambao utatumika katika usimamizi wa kodi kwa makundi ya walipakodi wenye vihatarishi na wasio na vihatarishi;
iv. Kuhakikisha taasisi yenye sura za utoaji wa huduma kwa pamoja ikiwemo vituo vya utoaji wa huduma kwa pamoja (one stop center) vilivyopo vinaboresha mifumo ya ukusanyaji kwa kuwezesha kutoa namba ya malipo jumuishi ili kurahisisha ulipaji kodi, ada na tozo mbalimbali kwa wateja na hivyo kuongeza uhiari wa ulipaji wa mapato ya Serikali;
v. Kutambua na kuanzisha vituo vipya vya utoaji wa huduma kwa pamoja kwa taasisi zote zenye huduma zinazoweza kutolewa kwa pamoja;
vi. Kulea walipakodi wapya kwa kuwapa elimu pamoja na kuweka mikakati ya urahisi wa utambuzi, usajili, ukadiriaji, na ulipaji wa kodi ya Serikali;
vii. Kuweka sera/mikakati ya kuchochea uchumi unaotumia miamala ya kielektroniki ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu (cash - lite economy);
viii. Kufanya mapitio ya vivutio vya kodi/misamaha ya kodi iliyotolewa ili kubaini faida na umuhimu wa kuendelea nayo au vinginevyo;
ix. Kuwarasimisha wafanyabiashara na watoa huduma wadogo kwa kuwatengea maeneo maalum na kuwapatia huduma muhimu za kijamii kwa lengo la kukuza biashara zao;
x. Kuendelea kutambua na kusajili kampuni za kimataifa zinazoendesha biashara za kidigitali nchini kwa kutumia mfumo wa usajili uliorahisishwa (simplified registration regime);
xi. Kuendelea kuwekeza kwenye matumizi ya teknolojia ili kuhakikisha mifumo ya Serikali inabadilishana taarifa;
xii. Kuendelea kutoa elimu ya ulipaji kodi kwa jamii kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, vituo vya huduma kwa walipakodi, kauli

mbiu za kitaifa, klabu za kodi mashuleni, kambi za jeshi za JKT mafunzo ya mgambo, na makongamano mbalimbali; na

xiii. Kuanzisha tuzo za uzalendo kupitia mfumo wa risiti za kielektroniki (EFD).

**2.3.2.1Misaada**

18. Katika mwaka 2024/25, misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 690.9. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 109.0 ni misaada ya kibajeti, shilingi bilioni 80.0 ni mifuko ya pamoja ya kisekta na shilingi bilioni 501.9 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za misaada zinazotarajiwa kutolewa kwa mwaka 2024/25 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zimepungua kwa asilimia 38 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,111.3 zilizoahidiwa mwaka 2023/24. Aidha, fedha za misaada zinatarajiwa kuendelea kupungua kwa kipindi cha muda wa kati ambapo mwaka 2026/27 zinatarajiwa kuwa shilingi bilioni 671.5, sawa na upungufu wa asilimia 3. Upungufu wa fedha za misaada unatokana na athari ya UVIKO - 19 na vita kati ya Urusi na Ukraine ambavyo vimeathiri ukuaji wa uchumi wa Nchi za Ulaya ambazo ni watoaji wakubwa wa misaada hiyo.

**2.3.2.2 Mikopo ya Ndani na Nje**

19. Katika kugharamia nakisi ya bajeti na kudhibiti mwenendo wa ongezeko la deni, Serikali itaendelea kutekeleza sera za bajeti ambazo zitawezesha ukuaji wa uchumi na kuhakikisha kuwa deni linaendelea kuwa himilivu. Katika mwaka 2024/25, Serikali inatarajia kukopa jumla ya shilingi bilioni 12,297.8 kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuziba nakisi ya bajeti ikilinganishwa na shilingi bilioni 11,895.7 zinazotarajiwa kukopwa mwaka 2023/24. Aidha, katika kipindi cha muda wa kati, nakisi ya bajeti inatarajiwa kuwa chini ya wastani wa asilimia 3.0 ya Pato la Taifa.

**a) Makadirio ya Mikopo ya Ndani**

20. Katika mwaka 2024/25, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 6,141.9. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 3,919.8 ni kwa ajili ya kulipia mikopo

itakayoiva na shilingi bilioni 2,222.1 ni kwa ajili ya kuziba nakisi ya bajeti. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaendelea kukopa kutoka vyanzo vya ndani kwa kiwango kisichozidi asilimia 1.0 ya Pato la Taifa kwa mwaka ili kutoathiri upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

**b) Makadirio ya Mikopo ya Nje**

21. Katika mwaka 2024/25, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 6,156.0 ikijumuisha mikopo yenye masharti nafuu shilingi bilioni 3,601.0 na mikopo yenye masharti ya kibiashara shilingi bilioni 2,555.0. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali inatarajia kukopa wastani wa shilingi bilioni 5,791.6 kwa mwaka.

#### 2.3.2.3 Mikakati ya Upatikanaji wa Misaada na Mikopo

22. Serikali itaendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kupitia Majadiliano ya Kimkakati (Strategic Dialogue) yanayolenga kuainisha vipaumbele vya Serikali ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo kama ilivyopangwa. Aidha, Serikali itatenga fedha za miradi inayotekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (counterpart fund) ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kama ilivyokusudiwa; pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali.

23. Serikali itaendelea kugharamia nakisi ya bajeti kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje kama itakavyoainishwa kwenye Mkakati wa Kusimamia Deni kwa kipindi cha Muda wa Kati (Medium Term Debt Management Strategy – MTDS) wa mwaka 2023. Aidha, Serikali itatumia mikopo yenye masharti nafuu (concessional loans) na ya kibiashara (non concessional loans) kugharamia miradi mikubwa ya kimkakati na yenye matokeo ya haraka kiuchumi. Vilevile, Serikali itaendelea kukopa kutoka vyanzo vya ndani kwa kutumia dhamana

za muda mfupi na mrefu kutoka kwenye soko la ndani la fedha na mitaji ili kugharamia nakisi ya bajeti ya Serikali.

### 2.3.3 Matumizi

24. Katika mwaka 2024/25, matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 47,424.9. Kati ya kiasi hicho, deni la Serikali shilingi bilioni 12,101.2, mishahara shilingi bilioni 11,774.8 na uendeshaji wa shughuli za Serikali shilingi bilioni 8,223.8. Aidha, matumizi kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 15,325.1 ikijumuisha ruzuku ya maendeleo (Elimumsingi na Sekondari bila ada na Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu). Katika kipindi cha muda wa kati, bajeti ya Serikali inatarajiwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 5.0. Maoteo ya bajeti ya Serikali katika muda wa kati yameainishwa katika **Jedwali Na. 2.1** hadi **2.5**.

#### 2.3.3.1 Mikakati ya Usimamizi wa Matumizi

25. Mikakati ya usimamizi wa matumizi katika kipindi cha muda wa kati itajumuisha yafuatayo:

i. Kuendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kudhibiti matumizi ikijumuisha mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu, malipo serikalini, ununuzi na usimamizi wa mali za Serikali;
ii. Kuelekeza fedha katika kukamilisha miradi ya kielelezo na kimkakati kwa kuhakikisha miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya;
iii. Kuimarisha uwajibikaji na udhibiti katika matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za umma ili kuziba mianya ya ubadhilifu kwa lengo la kupata thamani ya fedha katika matumizi ya Serikali; na
iv. Kuimarisha mfumo wa usimamizi na utendaji kazi katika taasisi na mashirika ya umma.

**Jedwali Na 2.1: Makadirio ya Bajeti katika Kipindi cha Muda wa Kati 2023/24 -2026/27 (Analytical Budget Frame)**

**Shilingi Bilioni**

| | 2023/24 BAJETI ILIYOIDHINISHWA | 2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI | 2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI | 2026/27 MAKADIRIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|
| **Jumla ya Mapato ya Ndani** | **31,381.0** | **34,436.2** | **36,497.5** | **38,957.0** |
| Mapato ya TRA (Kodi na Yasiyo Ya Kodi) | 26,725.4 | 29,520.7 | 31,113.3 | 33,126.8 |
| Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Taasisi na Mashirika) | 3,511.7 | 3,600.0 | 3,871.4 | 4,090.5 |
| Mapato ya Halmashauri | 1,143.9 | 1,315.5 | 1,512.8 | 1,739.7 |
| **Jumla ya Matumizi*** | **38,082.1** | **40,116.6** | **40,981.0** | **42,275.6** |
| Matumizi ya Kawaida | 24,004.8 | 26,025.5 | 27,014.4 | 27,754.0 |
| Malipo ya Riba Nje | 1,364.4 | 1,767.3 | 1,909.9 | 1,949.9 |
| Malipo ya Riba Ndani | 2,799.4 | 3,025.5 | 3,119.3 | 3,264.0 |
| Mishahara | 10,882.1 | 11,774.8 | 12,285.3 | 12,531.0 |
| Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii | 1,710.6 | 2,000.0 | 2,272.8 | 2,318.2 |
| Matumizi mengineyo | 6,065.0 | 6,223.8 | 6,276.5 | 6,532.2 |
| Ruzuku ya Maendeleo | 1,183.4 | 1,234.1 | 1,150.6 | 1,158.6 |
| -Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | 783.7 | 832.4 | 746.1 | 751.3 |
| -Elimumsingi na Sekondari Bila Ada | 399.6 | 401.6 | 404.5 | 407.3 |
| Matumizi ya Maendeleo | 14,077.2 | 14,091.1 | 13,966.6 | 14,521.7 |
| Fedha za Ndani | 10,795.1 | 10,650.2 | 10,625.9 | 11,189.0 |
| Fedha za Nje | 3,282.1 | 3,440.8 | 3,340.7 | 3,332.7 |
| **Nakisi ya Bajeti bila ya Kujumlisha Misaada** | **(6,701.0)** | **(5,680.4)** | **(4,483.4)** | **(3,318.7)** |
| **Misaada** | **1,111.3** | **690.9** | **679.5** | **671.3** |
| Misaada ya Kibajeti | 56.4 | 109.0 | 99.2 | 98.7 |
| Misaada ya Maendeleo | 924.8 | 501.9 | 500.4 | 495.9 |
| Mifuko ya Kisekta | 130.1 | 80.0 | 79.9 | 76.7 |
| **Nakisi ya Bajeti Ikijumuisha Misaada** | **(5,589.7)** | **(4,989.5)** | **(3,803.9)** | **(2,647.4)** |
| **Jumla ya Nakisi** | **(5,589.7)** | **(4,989.5)** | **(3,803.9)** | **(2,647.4)** |
| **Kuziba Nakisi** | **5,589.7** | **4,989.5** | **3,803.9** | **2,647.4** |
| **Kuziba Nakisi Kutoka Nje** | **3,691.4** | **2,767.4** | **1,374.7** | **171.1** |
| Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 2,127.8 | 742.0 | 388.0 | - |
| Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo | 2,227.1 | 2,812.1 | 2,713.6 | 2,715.2 |
| Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta | - | 46.9 | 46.8 | 44.9 |
| Mikopo ya Kibiashara | 2,100.5 | 2,555.0 | 2,635.1 | 2,675.4 |
| Malipo ya Mtaji Deni la Nje | (2,763.9) | (3,388.5) | (4,408.7) | (5,264.5) |
| **Kuziba Nakisi Kutoka Ndani** | **1,898.3** | **2,222.1** | **2,429.2** | **2,476.3** |
| Mkopo kwa ajili kugharamia miradi ya maendeleo (NDF) | **1,898.3** | **2,222.1** | **2,429.2** | **2,476.3** |
| Mkopo kwa ajili ya kulipa mtaji | 3,542.1 | 3,919.8 | 4,042.0 | 3,858.4 |
| Malipo ya Mtaji Deni la Ndani (Rollover) | (3,542.1) | (3,919.8) | (4,042.0) | (3,858.4) |
| **Pato Ghafi la Taifa** | **210,276.2** | **223,149.7** | **233,769.3** | **249,072.2** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

Tanbihi: Kiasi cha jumla ya matumizi hakijumuishi malipo ya mtaji

**Jedwali Na 2.2 Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato la Taifa kwa Kipindi cha Muda wa Kati (Analytical Budget Frame)**

| | 2023/24 BAJETI ILIYOIDHINISHWA | 2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI | 2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI | 2026/27 MAKADIRIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| **Jumla ya Mapato ya Ndani** | **14.9%** | **15.4%** | **15.6%** | **15.6%** |
| Mapato ya TRA (Kodi na Yasiyo Ya Kodi) | 12.7% | 13.2% | 13.3% | 13.3% |
| Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Taasisi na Mashirika) | 1.7% | 1.6% | 1.7% | 1.6% |
| Mapato ya Halmashauri | 0.5% | 0.6% | 0.6% | 0.7% |
| | | | | |
| **Jumla ya Matumizi*** | **18.1%** | **18.0%** | **17.5%** | **17.0%** |
| Matumizi ya Kawaida | 11.4% | 11.7% | 11.6% | 11.1% |
| Malipo ya Riba Nje | 0.6% | 0.8% | 0.8% | 0.8% |
| Malipo ya Riba Ndani | 1.3% | 1.4% | 1.3% | 1.3% |
| Mishahara | 5.2% | 5.3% | 5.3% | 5.0% |
| Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii | 0.8% | 0.9% | 1.0% | 0.9% |
| Matumizi mengineyo | 2.9% | 2.8% | 2.7% | 2.6% |
| Ruzuku ya Maendeleo | | | | |
| -Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | 0.4% | 0.4% | 0.3% | 0.3% |
| -Elimumsingi na Sekondari Bila Ada | 0.2% | 0.2% | 0.2% | 0.2% |
| Matumizi ya Maendeleo | 6.7% | 6.3% | 6.0% | 5.8% |
| Fedha za Ndani | 5.1% | 4.8% | 4.5% | 4.5% |
| Fedha za Nje | 1.6% | 1.5% | 1.4% | 1.3% |
| | | | | |
| **Nakisi ya Bajeti bila ya Kujumlisha Misaada** | **-3.2%** | **-2.5%** | **-1.9%** | **-1.3%** |
| | | | | |
| **Misaada** | **0.5%** | **0.3%** | **0.3%** | **0.3%** |
| Misaada ya Kibajeti | 0.0% | 0.0% | 0.0% | 0.0% |
| Misaada ya Maendeleo | 0.4% | 0.2% | 0.2% | 0.2% |
| Mifuko ya Kisekta | 0.1% | 0.0% | 0.0% | 0.0% |
| | | | | |
| **Nakisi ya Bajeti Ikijumuisha Misaada** | **-2.7%** | **-2.2%** | **-1.6%** | **-1.1%** |
| | | | | |
| **Jumla ya Nakisi** | **-2.7%** | **-2.2%** | **-1.6%** | **-1.1%** |
| | | | | |
| **Kuziba Nakisi** | **2.7%** | **2.2%** | **1.6%** | **1.1%** |
| **Kuziba Nakisi Kutoka Nje** | **1.8%** | **1.2%** | **0.6%** | **0.1%** |
| Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 1.0% | 0.3% | 0.2% | 0.0% |
| Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo | 1.1% | 1.3% | 1.2% | 1.1% |
| Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta | 0.0% | 0.0% | 0.0% | 0.0% |
| Mikopo ya Kibiashara | 1.0% | 1.1% | 1.1% | 1.1% |
| Malipo ya Mtaji Deni la Nje | -1.3% | -1.5% | -1.9% | -2.1% |
| **Kuziba Nakisi Kutoka Ndani** | **0.9%** | **1.0%** | **1.0%** | **1.0%** |
| Mkopo kwa ajili kugharamia miradi ya maendeleo (NDF) | **0.9%** | **1.0%** | **1.0%** | **1.0%** |
| Mkopo kwa ajili ya kulipa mtaji | 1.7% | 1.8% | 1.7% | 1.5% |
| Malipo ya Mtaji Deni la Ndani (Rollover) | -1.7% | -1.8% | -1.7% | -1.5% |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

**Jedwali Na 2.3: Makadirio ya Bajeti katika Kipindi cha Muda wa Kati 2023/24 -2026/27 (Accounting Budget Frame), Shilingi Bilioni**

| | 2023/24 BAJETI ILIYOIDHINISHWA | 2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI | 2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI | 2026/27 MAKADIRIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| **I. JUMLA YA MAPATO** | **44,388.1** | **47,424.9** | **49,431.7** | **51,398.5** |
| | | | | |
| Mapato ya Ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri | 31,381.0 | 34,436.2 | 36,497.5 | 38,957.0 |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 2,184.1 | 851.0 | 487.2 | 98.7 |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi | 3,152.0 | 3,314.0 | 3,214.0 | 3,211.1 |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta | 130.1 | 126.9 | 126.7 | 121.6 |
| Mikopo ya Ndani - Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover) | 3,542.1 | 3,919.8 | 4,042.0 | 3,858.4 |
| Mikopo ya Ndani ya Kibiashara (NDF) | 1,898.3 | 2,222.1 | 2,429.2 | 2,476.3 |
| Mikopo ya Nje ya Kibiashara | 2,100.5 | 2,555.0 | 2,635.1 | 2,675.4 |
| | | | | |
| **II. JUMLA YA MATUMIZI** | **44,388.1** | **47,424.9** | **49,431.7** | **51,398.5** |
| | | | | |
| **Matumizi ya Kawaida** | 30,310.8 | 33,333.8 | 35,465.1 | 36,876.8 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 12,771.5 | 14,716.0 | 16,370.9 | 17,291.8 |
| o/w Malipo ya riba | 4,163.8 | 4,792.8 | 5,029.2 | 5,213.9 |
| o/w Malipo ya mtaji | 6,306.0 | 7,308.3 | 8,450.7 | 9,122.9 |
| Mishahara | 10,882.1 | 11,774.8 | 12,285.3 | 12,531.0 |
| Matumizi Mengineyo | 5,473.8 | 5,608.9 | 5,658.3 | 5,895.5 |
| Ruzuku ya Maendeleo | 1,183.4 | 1,234.1 | 1,150.6 | 1,158.6 |
| | | | | |
| **Matumizi ya Maendeleo** | 14,077.2 | 14,091.1 | 13,966.6 | 14,521.7 |
| Fedha za Ndani | 10,795.1 | 10,650.2 | 10,625.9 | 11,189.0 |
| Fedha za Nje | 3,282.1 | 3,440.8 | 3,340.7 | 3,332.7 |
| | | | | |
| **Pato Ghafi la Taifa** | **210,276.2** | **223,149.7** | **233,769.3** | **249,072.2** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

Tanbihi: Kiasi cha jumla ya matumizi kinajumuisha malipo ya mtaji

**Jedwali Na 2.4: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato la Taifa kwa Kipindi cha Muda wa Kati 2023/24 -2026/27 (Accounting Budget Frame)**

| | 2023/24 BAJETI ILIYOIDHINISHWA | 2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI | 2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI | 2026/27 MAKADIRIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| **I. JUMLA YA MAPATO** | **21.1%** | **21.3%** | **21.1%** | **20.6%** |
| | | | | |
| Mapato ya Ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri | **14.9%** | **15.4%** | **15.6%** | **15.6%** |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti | **1.0%** | **0.4%** | **0.2%** | **0.0%** |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi | **1.5%** | **1.5%** | **1.4%** | **1.3%** |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta | **0.1%** | **0.1%** | **0.1%** | **0.0%** |
| Mikopo ya Ndani - Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover) | **1.7%** | **1.8%** | **1.7%** | **1.5%** |
| Mikopo ya Ndani ya Kibiashara (NDF) | **0.9%** | **1.0%** | **1.0%** | **1.0%** |
| Mikopo ya Nje ya Kibiashara | **1.0%** | **1.1%** | **1.1%** | **1.1%** |
| | | | | |
| **II. JUMLA YA MATUMIZI** | **21.1%** | **21.3%** | **21.1%** | **20.6%** |
| | | | | |
| **Matumizi ya Kawaida** | **14.4%** | **14.9%** | **15.2%** | **14.8%** |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | **6.1%** | **6.6%** | **7.0%** | **6.9%** |
| o/w Malipo ya riba | **2.0%** | **2.1%** | **2.2%** | **2.1%** |
| o/w Malipo ya mtaji | **3.0%** | **3.3%** | **3.6%** | **3.7%** |
| Mishahara | **5.2%** | **5.3%** | **5.3%** | **5.0%** |
| Matumizi Mengineyo | **2.6%** | **2.5%** | **2.4%** | **2.4%** |
| Ruzuku ya Maendeleo | **0.6%** | **0.6%** | **0.5%** | **0.5%** |
| | | | | |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **6.7%** | **6.3%** | **6.0%** | **5.8%** |
| Fedha za Ndani | **5.1%** | **4.8%** | **4.5%** | **4.5%** |
| Fedha za Nje | **1.6%** | **1.5%** | **1.4%** | **1.3%** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

## Jedwali Na 2.5: Mgawanyo wa Bajeti Kisekta kwa Kipindi cha Muda wa Kati (Shilingi Bilioni)

| SEKTA | NAMBA YA SEKTA | 2023/24 BAJETI ILIYOIDHINISHWA | 2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI | 2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI | 2026/27 MAKADIRIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|
| **1 - Elimu** | **709** | **5,979.7** | **6,227.4** | **6,338.3** | **6,534.0** |
| 1.1 - Elimu Msingi | 7091,7092 | 4,485.1 | 4,670.9 | 4,754.0 | 4,900.8 |
| 1.2 - Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 7,093 | 144.4 | 150.4 | 153.1 | 157.8 |
| 1.3 - Elimu ya Juu | 7,094 | 1,165.9 | 1,214.2 | 1,235.8 | 1,274.0 |
| 1.4 - Sayansi, Teknolojia na Ubunifu | 7,098 | 61.4 | 63.9 | 65.1 | 67.1 |
| 1.5 - Huduma za Utawala | 7,098 | 122.9 | 128.0 | 130.3 | 134.3 |
| **2 - Afya** | **707** | **2,463.7** | **2,565.8** | **2,611.2** | **2,691.8** |
| 2.1 - Huduma za Tiba | '071,7072,7073,7074,7075,7076 | 978.1 | 1,018.6 | 1,036.7 | 1,068.7 |
| 2.2 - Huduma za Kinga | 7071,7073,7074,7076 | 308.1 | 320.9 | 326.6 | 336.7 |
| 2.3 - Hospitali za Rufaa za Mikoa | 7071,7072,7073,7074 | - | - | - | - |
| 2.4 - Zahanati | 7071,7072,7073,7074,7075 | 92.8 | 96.6 | 98.3 | 101.3 |
| 2.5 - Vituo vya Afya | 7071,7072,7073,7074,7075 | 155.2 | 161.7 | 164.5 | 169.6 |
| 2.6 - Hospitali za Wilaya | 7071,7072,7073,7074,7075 | 821.9 | 855.9 | 871.1 | 898.0 |
| 2.7 - Huduma za Utawala | 7,076 | 107.6 | 112.1 | 114.0 | 117.5 |
| **3 - Huduma za Utawala na Deni la Serikali** | **701** | **11,788.3** | **12,733.2** | **13,110.9** | **13,545.1** |
| 3.1 - Mihimili | 7,011 | 4,185.7 | 4,359.1 | 4,436.6 | 4,573.6 |
| 3.2 - Usimamizi wa mapato na Matumizi | 7,011 | 3,191.2 | 3,323.4 | 3,382.5 | 3,486.9 |
| 3.3 - Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimataifa | 7,011 | 247.7 | 257.9 | 262.6 | 270.7 |
| 3.4 - Deni la Serikali (Malipo ya Riba) | 7,018 | 4,163.8 | 4,792.8 | 5,029.2 | 5,213.9 |
| **4 - Ulinzi, Utawala wa Sheria na Usalama** | **703** | **4,688.3** | **4,882.5** | **4,969.2** | **5,122.6** |
| 4.1 - Ulinzi | 702 | 2,987.3 | 3,111.0 | 3,166.3 | 3,264.1 |
| 4.2 - Usalama wa Umma | 7,036 | 413.3 | 430.5 | 438.1 | 451.6 |
| 4.3 - Mahakama | 7,033 | 1,287.7 | 1,341.0 | 1,364.8 | 1,406.9 |
| **5 - Maendeleo ya Uchumi** | **704** | **9,470.1** | **9,862.4** | **10,037.9** | **10,347.8** |
| 5.1 - Kilimo | 7,042 | 1,465.2 | 1,525.9 | 1,553.1 | 1,601.1 |
| 5.2 - Madini | 7,044 | 89.3 | 93.0 | 94.6 | 97.5 |
| 5.3 - Nishati | 7,043 | 3,048.6 | 3,174.9 | 3,231.4 | 3,331.2 |
| 5.4 - Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano | 7045, 7046 | 3,844.6 | 4,003.9 | 4,075.1 | 4,200.9 |
| 5.5 - Maliasili, Utalii na Mazingira | 7,049 | 649.1 | 676.0 | 688.1 | 709.3 |
| 5.6 - Viwanda | 7,047 | 110.4 | 115.0 | 117.0 | 120.6 |
| 5.7 - Biashara | 7,047 | 242.5 | 252.5 | 257.0 | 264.9 |
| 5.8 - Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi | 7,041 | 20.3 | 21.2 | 21.6 | 22.3 |
| **6 - Hifadhi ya Jamii** | **710** | **2,345.4** | **2,442.6** | **2,485.9** | **2,562.7** |
| 6.1 - Wazee, Watoto na Watu wenye Ulemavu | 7101,7102 | 52.2 | 54.4 | 55.3 | 57.0 |
| 6.2 - Mifuko ya Hifadhi ya Jamii | 7,109 | 1,847.3 | 1,923.9 | 1,958.0 | 2,018.5 |
| 6.3 - Mfuko wa Bima wa Afya | 7,109 | 445.9 | 464.3 | 472.6 | 487.2 |
| **7 - Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii** | **706** | **1,346.7** | **1,402.4** | **1,427.6** | **1,471.7** |
| 7.1 - Maji | 7,063 | 766.2 | 797.9 | 812.2 | 837.3 |
| 7.2 - Ardhi, Nyumba na Makazi ya Watu | 7,065 | 175.3 | 182.5 | 185.8 | 191.5 |
| 7.3 - Maendeleo ya Jamii | 7,062 | 369.8 | 385.1 | 392.0 | 404.1 |
| 7.4 - Habari, Michezo na Utamaduni | 7,081 | 35.4 | 36.9 | 37.6 | 38.8 |
| **Jumla ya Sekta** | | **38,082.1** | **40,116.3** | **40,981.0** | **42,275.7** |
| | | | | | |
| Deni la Serikali (Ulipaji wa Mtaji) | | 6,306.0 | 7,308.3 | 8,450.7 | 9,122.9 |
| | | | | | |
| Jumla Kuu | | **44,388.1** | **47,424.7** | **49,431.7** | **51,398.6** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha



# 3 USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI



# 3

# USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

## 3. USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

Sehemu hii inaelezea vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25. Usimamizi wa Vihatarishi katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma unasaidia kubaini maeneo mahsusi yenye vihatarishi yatakayofanyiwa uchambuzi, ufuatiliaji, tathmini ya kina pamoja na mikakati ya kukabiliana na athari zitakazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali.

### 3.1 Vihatarishi vya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti

26. Katika utekelezaji wa mpango na bajeti vipo vihatarishi vinavyoweza kutokea na kuathiri ufikiaji wa malengo yaliyokusudiwa. Hivyo, ni muhimu kuelewa vyanzo na aina ya vihatarishi ambavyo vinaweza kuathiri utekelezaji wa mpango na bajeti ili kuweza kuchukua hatua za kukabiliana navyo. Vihatarishi hivyo, vinaweza kuwa katika kipindi cha muda mfupi, kati au mrefu. Kwa muktadha wa Mpango na Bajeti vihatarishi vimebainishwa katika makundi matatu kutokana na asili yake ambavyo ni vihatarishi vya: Uchumi Jumla, Madeni Sanjari, na Mtambuka.

#### 3.1.1 Vihatarishi vya Uchumi Jumla

27. Baadhi ya vihatarishi vya uchumi jumla ni pamoja na ukuaji wa uchumi, mabadiliko ya bei za bidhaa, viwango vya kubadilisha fedha, riba, akiba ya fedha za kigeni na uhimilivu wa sekta ya fedha. Athari zinazoweza kusababishwa na vihatarishi hivyo ni kama ifuatavyo:

**a) Ukuaji wa Uchumi:** Ukusanyaji wa mapato kwa kiasi kikubwa hutegemea ukuaji wa uchumi. Endapo mdororo wa uchumi wa dunia ukitokea kama ilivyokuwa katika kipindi cha mwaka 2020 – 2022, utaathiri ukuaji wa uchumi wa ndani ambao utasababisha kutokufikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato na upatikanaji wa mikopo na misaada ili kuziba nakisi ya bajeti. Aidha, mdororo wa uchumi unaweza kuathiri uhimilivu wa

deni la Serikali katika kipindi cha muda mrefu na hivyo kuifanya Serikali kukosa sifa za kukopesheka.

**b)** **Mabadiliko ya Bei za Bidhaa:** Kushuka kwa bei za bidhaa zinazouzwa nje kama dhahabu na bidhaa asilia, inaweza kupunguza mapato yatokanayo na mauzo nje ya nchi hivyo kuongeza nakisi ya bajeti na upungufu wa fedha za kigeni. Aidha, kupanda kwa bei za bidhaa muhimu katika soko la dunia, hususan mafuta ya dizeli, petroli na mbolea kutaongeza: matumizi ya fedha za kigeni kugharamia bidhaa hizo, gharama za uzalishaji katika sekta binafsi, uendeshaji wa shughuli za Serikali na shinikizo la mfumuko wa bei nchini.

**c)** **Mabadiliko ya Viwango vya Kubadilisha Fedha:** Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kutaathiri utekelezaji wa bajeti kwa kuongeza matumizi kwa ajili ya ugharamiaji wa malipo ya nje, hususan utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo kiasi kikubwa hutegemea bidhaa mtaji kutoka nje. Aidha, athari nyingine inaweza kutokea kwenye ulipaji wa deni la nje la Serikali.

**d)** **Mabadiliko ya Riba za Mikopo:** Kupanda kwa viwango vya riba za mikopo ya ndani na nje kutaongeza malipo ya riba za mikopo na hivyo kutofikiwa kwa malengo ya ukopaji.

**e)** **Akiba ya Fedha za Kigeni:** Upungufu wa fedha za kigeni duniani, hasa dola ya Marekani ambayo inashikilia zaidi ya asilimia 80 ya biashara za kimataifa, umechagizwa na janga la UVIKO-19, vita kati ya Urusi na Ukraine, mabadiliko ya tabianchi na sera za fedha za Marekani. Sababu hizo zimesababisha kupanda kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali ikiwemo usafirishaji, na hivyo kuongeza mahitaji ya dola; kuvurugika kwa mfumo wa ugavi, wawekezaji wengi kuwekeza dola zao Marekani. Kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni nchini kutapunguza uwezo wa Serikali kufanya malipo ya nje kwa ajili ya kugharamia mahitaji muhimu. Mahitaji hayo ni pamoja na

petroli, dawa na malighafi muhimu za uzalishaji nchini na hivyo kuleta athari katika ukuaji wa uchumi, makusanyo ya kodi, na utoaji huduma.

f) **Uhimilivu wa Sekta ya Fedha:** Kuanguka kwa sekta ndogo ya benki kunaweza kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuporomoka kwa thamani ya rasilimali za benki, ukwasi usioweza kukidhi mahitaji ya kila siku ya wenye amana na wakopaji, kupungua kwa mtaji wa benki, kuyumba kwa sekta binafsi na kusababisha kuongezeka kwa mikopo chechefu. Endapo hali hii itatokea, benki zitakosa uwezo wa kutoa mikopo kwa sekta binafsi na hivyo kupelekea sekta binafsi kudorora, kupungua kwa ajira na uzalishaji na kuathiri wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

### 3.1.2 Vihatarishi vya Madeni Sanjari

28. Madai yanayotokana na amri za mahakama yanaweza kuongeza matumizi ya Serikali nje ya mpango na bajeti. Aidha, Serikali imekuwa ikitoa dhamana kwa mashirika ya umma ili yaweze kukopa katika mabenki na taasisi mbalimbali za kifedha kwa lengo la kuwekeza katika miradi ya maendeleo. Shirika la umma lililopewa dhamana likishindwa kurejesha mkopo, Serikali italazimika kurejesha mkopo huo na hivyo kuathiri utekelezaji wa bajeti.

### 3.1.3 Vihatarishi Mtambuka

29. Baadhi ya vihatarishi mtambuka vinahusisha siasa na mahusiano ya kidiplomasia, mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko, pamoja na udanganyifu wa kifedha. Athari zinazoweza kusababishwa na vihatarishi hivyo ni kama ifuatavyo:

a) **Siasa na Mahusiano ya Kidiplomasia**: Kuvunjika kwa mahusiano ya kidiplomasia pamoja na migogoro ya kisiasa duniani inaweza kuathiri utekelezaji wa bajeti kutokana na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi, kuhitajika kwa gharama kuhudumia wakimbizi, ulinzi wa mipaka ya nchi na kupungua kwa misaada.

b) **Mabadiliko ya Tabianchi, Majanga ya Asili na Magonjwa ya Mlipuko:** Vihatarishi hivyo vinahusisha tetemeko la ardhi, ukame, vimbunga, mafuriko na magonjwa ya mlipuko. Vihatarishi hivyo vikitokea vitasababisha kukwama kwa shughuli za kiuchumi, uharibifu wa miundombinu na vifo. Aidha, itailazimu Serikali kuhitaji bajeti ya ziada ili kutoa msaada wa dharura kwa waliothirika ikiwamo urejeshaji wa miundombinu iliyoharibika, dawa na chakula.

c) **Udanganyifu wa Kifedha:** Wakati wa utekelezaji wa makujumu ya Serikali, kuna uwezekano wa kutokea kwa vitendo vya udanganyifu ambavyo vinaweza kuisababishia Serikali kutofikia malengo tarajiwa na kuleta taswira hasi. Vitendo vya udanganyifu vinavyoweza kutokea ni pamoja na kuchepusha mapato ya Serikali katika mifumo ya kielekroniki ya ukusanyaji mapato, kuingia mikataba isiyo na maslahi ya taifa ili kupata manufaa binafsi, matumizi ya mali za umma kwa faida binafsi, rushwa, wizi wa fedha na mali na kughushi nyaraka za Serikali na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

### 3.2 Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi

30. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza ili kuhakikisha malengo na shabaha za utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2024/25 yanafikiwa. Hatua hizo ni pamoja na:

i. Kuendelea kutekeleza na kusimamia sera ya fedha na bajeti kwa kuzingatia malengo na shabaha za kiuchumi;
ii. Kuongeza ufanisi katika uandaaji wa maoteo ya viashiria vya uchumi jumla kwa kujumuisha vihatarishi;
iii. Kuainisha vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti pamoja na mikakati ya kukabiliana navyo;

iv. Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa na Kusimamia Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi Katika Taasisi za Umma;
v. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 ili kutoa dhamana kwenye miradi yenye tija;
vi. Kuboresha mazingira ya uwekezaji wa ndani na nje ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na bidhaa za viwandani ili kupunguza nakisi ya bajeti kwa kuhakikisha ongezeko la matumizi ya Serikali linakwenda sambamba na ongezeko la mapato yatokanayo na uzalishaji;
vii. Kuendelea kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ili kupunguza utegemezi wa kilimo kinachotegemea mvua na hivyo kuwa na uhakika wa kuvuna na kuongeza kiwango cha uzalishaji;
viii. Kuimarisha hifadhi ya chakula ya Taifa kwa ajili ya tahadhari ya kukabiliana na mahitaji ya upungufu wa chakula na kudhibiti mfumuko wa bei;
ix. Kuendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tahadhari katika taasisi zote za umma ili kubaini changamoto zinazoweza kujitokeza na kuwezesha maamuzi ya kiutendaji kufanyika kwa wakati;
x. Kuimarisha matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza utegemezi wa mafuta yanayoagizwa kutoka nje na kudhibiti uharibifu wa mazingira;
xi. Kuendelea kuimarisha mahusiano ya kiuchumi ya kikanda na kimataifa ili kuongeza wigo wa ushirikiano pamoja na masoko ya bidhaa na huduma;
xii. Kuendelea kutoa elimu ya kukabiliana na majanga mbalimbali ikiwemo milipuko ya magonjwa, uvamizi wa wanyama, wadudu na ndege waharibifu;
xiii. Kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria;
xiv. Kutekeleza mikakati ya kisekta kuhusu upatikanaji wa fedha za kigeni na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni;

xv. Kuendelea kuimarisha na kusimamia Mfuko wa Taifa wa Maafa ili kukabiliana na athari za majanga pindi yanapotokea;

xvi. Kuimarisha usimamizi wa mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji mapato, kuongeza udhibiti wa mifumo na kuimarisha usimamizi wa Mwongozo wa Uandaaji na Utekelezaji wa Usimamizi wa Vitaharishi vya Udanganyifu katika Sekta ya Umma; na

xvii. Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa mikakati inayolenga kuimarisha ustawi wa sekta ya benki kwa: kufanya uwekezaji kwenye maeneo yenye tija, kupunguza kiwango cha mikopo chechefu, kuhimiza mabenki kuongeza umakini katika kuidhinisha mikopo kwa kufuata miongozo iliyopo pamoja na kuzitaka benki kuwasilisha na kutumia taarifa za wakopaji kwenye kanzidata ya taarifa za wakopaji.



# 4 MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

# 4

# MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

## 4. MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

Sehemu hii inatoa maelekezo ya jumla na maelekezo mahsusi yanayopaswa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli katika hatua zote za uandaaji, uwasilishaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2024/25. Aidha, wakati wa maandalizi ya mpango na bajeti Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyorejewa katika mwongozo huu. Vile vile, wanaelekezwa kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka 2023/24 ili kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza na kuandaa mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo kwa lengo la kuboresha uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2024/25.

### 4.1 Maandalizi ya Mpango na Bajeti

31. Wakati wa maandalizi ya mpango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia malengo na shabaha za Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2024/25, mipango mikakati ya taasisi wanazosimamia na maelekezo mengine yanayotolewa na Serikali.

#### 4.1.1 Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti

32. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kuanza maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Muda wa Kati (MTEF) mara baada ya kuidhinishwa kwa mwongozo huu. Vitabu vya bajeti ya muda wa kati vya mafungu vitawasilishwa Wizara ya Fedha wiki ya nne ya Januari 2024. Vitabu vya bajeti ya muda wa kati vya Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma viwasilishwe Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya uchambuzi kwa kuzingatia ratiba itakayotolewa. Aidha, vitabu vya bajeti ya muda wa kati vya Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa vitawasilishwa Wizara ya Fedha baada ya uchambuzi wa OR-

TAMISEMI. Vile vile, mafungu yataandaa randama za bajeti zitakazowasilishwa kwenye Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuzingatia ratiba itakayotolewa na Ofisi ya Bunge. Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4.1**.

**Jedwali Na. 4.1: Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25**

| Mwezi | Shughuli |
|---|---|
| **Agosti – Novemba 2023** | Maandalizi na uidhinishwaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali |
| **Novemba 2023** | Usambazaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali |
| **Novemba 2023 - Februari 2024** | Maandalizi ya mipango na bajeti za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali; Ofisi za Wakuu wa Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi na Mashirika ya Umma |
| **Februari – Machi 2024** | Wizara ya Fedha kufanya uchambuzi wa mipango na bajeti za kisekta na kwa mafungu |
| **Machi 2024** | Mafungu kuwasilisha mipango na bajeti kwenye Kamati za Kisekta za Bunge |
| **Aprili – Juni 2024** | Mafungu kuwasilisha mipango na bajeti bungeni |
| **Juni 2024** | Serikali kuwasilisha bungeni Sheria ya Fedha na Sheria ya Matumizi |
| **1 Julai 2024 - 30 Juni 2025** | Mafungu kuanza utekelezaji wa mipango na bajeti kama ilivyoidhinishwa na Bunge |

#### 4.1.2 Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya Kibajeti

33. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha kuwa, uingizaji wa takwimu sahihi za bajeti kwenye mifumo ya CBMS na PlanRep kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma unazingatia muda uliopangwa ikiwemo mambo muhimu yafuatayo:

i. Usahihi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa kuzingatia ukomo wa bajeti kwa mwaka 2024/25 na makisio yanayoonesha uhalisia kulingana na ukomo wa miaka miwili inayofuata (2025/26 hadi 2026/27);

ii. Matumizi sahihi ya namba za miradi zinazotolewa na Wizara ya Fedha, mageresho ya kibajeti (GFS codes 2014) na vizio vya vipimo kama vilivyoainishwa kwenye mifumo;

iii. Kuhakikisha kuwa takwimu za bajeti ya matumizi ya kawaida zinazoingizwa kama *transfers* zinagawanywa kati ya matumizi mengineyo na mishahara na kuingizwa kwenye idara na vitengo husika;

iv. Kuingiza viwango sahihi vya stahili za kisheria ikiwemo posho, pango, umeme, simu na maji kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR – MUUUB); na

v. Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kutumia mfumo wa kibajeti wa PlanRep kwa ajili ya maandalizi ya mipango na bajeti ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa.

#### 4.1.3 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Mpango na Bajeti

34. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia ratiba ya maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2024/25 inayoonesha muda wa maandalizi, uingizaji wa takwimu za bajeti ya Serikali kwenye mifumo ya CBMS na PlanRep na uwasilishaji wa vitabu vya Bajeti ya Muda wa Kati wa Matumizi (MTEF) na Randama.

**a) Uwasilishaji wa MTEF**

35. Wakati wa uwasilishaji wa mpango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

i. Muundo wa uwasilishaji wa MTEF kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1D**;
ii. Ratiba ya uwasilishaji wa mpango na bajeti;
iii. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha nakala mango (hard copy) mbili (2) ya makadirio ya mapato na matumizi ya fungu husika, siku tano (5) kabla ya kuanza uchambuzi kwa kuzingatia ratiba ya uchambuzi;
iv. Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma yanapaswa kuwasilisha nakala tete (soft copy) ya makadirio ya mapato na matumizi Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kuzingatia ratiba itakayotolewa na Ofisi ya Msajili wa Hazina;
v. Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinapaswa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi OR-TAMISEMI kwa kuzingatia ratiba itakayotolewa na OR-TAMISEMI; na
vi. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinatakiwa kuwasilisha nakala mango moja (1) na nakala tete Wizara ya Fedha, OR –TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina zilizofanyiwa marekebisho ndani ya siku tano (5) baada bajeti ya fungu husika kuidhinishwa na Bunge.

**b) Uwasilishaji wa Randama**

36. Maafisa Masuuli wa mafungu wanaelekezwa kuwasilisha randama kwa Katibu wa Bunge na nakala Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kabla au ifikapo tarehe 10 Machi, 2024 kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge (Toleo la Mwaka 2023). Aidha, Maafisa Masuuli wa mafungu wanaelekezwa kuwasilisha randama za utekelezaji wa Mwaka 2023/24 na mpango na bajeti wa Mwaka 2024/25 kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za

Kisekta kwa kuzingatia ratiba ya vikao vya kamati husika itakayotolewa na Katibu wa Bunge. Muundo wa uwasilishaji wa MTEF ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1E.**

## 4.2 Maelekezo ya Jumla ya Uandaaji wa Mpango na Bajeti

37. Sehemu hii inatoa maelekezo ya ujumla kuhusu Kamati za Bajeti, viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, mkakati wa kuongeza fedha za kigeni na mapato. Maeneo mengine ni udhibiti wa uzalishaji na ulimbikizaji wa madeni, uandaaji wa bajeti ya mishahara, uendeshaji wa ofisi na maendeleo.

### 4.2.1 Kamati za Bajeti

38. Katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha:

i. Kamati za Bajeti zinaimarishwa na wajumbe wote kushiriki kikamilifu katika kuandaa na kutekeleza bajeti kwa mujibu wa Kifungu 18(2) na Kanuni ya 17(3) ya Sheria ya Bajeti, Sura 439;

ii. Vikao vya Kamati za Bajeti vinafanyika wakati wa maandalizi ya mpango na bajeti; ugawaji wa rasilimali fedha zilizopokelewa/kukusanywa; na kupitia taarifa za ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa mpango na bajeti; na

iii. Muhtasari wa vikao hivyo unaandaliwa kwa kuzingatia muundo uliobainishwa kwenye **Kiambatisho Na. 1F** cha mwongozo huu na kuwasilishwa Wizara ya Fedha kila robo mwaka.

### 4.2.2 Mikakati ya Kuongeza Mapato

39. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa na mikakati ya kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa kufanya yafuatayo:

i. Kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuongeza mapato katika maeneo wanayosimamia kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo na kuwasilisha Wizara ya Fedha;

ii. Kuwajengea uwezo viongozi na watendaji kuhusu mbinu za ukusanyaji wa mapato, uzuiaji wa mianya ya upotevu na uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato;
iii. Kuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa yanaingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mujibu wa matakwa ya Kifungu 58(a) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 isipokuwa pale ilipoelekezwa vinginevyo kwa mujibu wa Sheria husika;
iv. Kuhakikisha matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ya Serikali ya ukusanyaji wa mapato kwa kufanya uhakiki na ukaguzi wa mifumo mara kwa mara ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;
v. Kuandaa na kuhuisha kanzidata na takwimu za vyanzo vyote vya mapato katika ngazi ya kata, vijiji na mitaa kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji na kudhibiti upotevu wa mapato;
vi. Kuzingatia sheria za kodi ikiwa ni pamoja na kutoza kodi ya zuio (withholding tax) na kudai risiti za kielektroniki kwa malipo yote yanayofanywa kwa wazabuni na wakandarasi;
vii. Kuwasilisha Wizara ya Fedha kila mwezi taarifa za makusanyo kutoka kila chanzo cha mapato kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa lengo la kutathmini mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali;
viii. Kuhakikisha vituo vya utoaji wa huduma kwa pamoja vilivyopo vinaboresha mifumo ya ukusanyaji kwa kuwezesha kutoa namba ya malipo jumuishi ili kurahisisha ulipaji kodi, ada na tozo mbalimbali kwa wateja na hivyo kuongeza uhiari wa ulipaji wa mapato ya Serikali;
ix. Kutambua na kuanzisha vituo vipya vya utoaji wa huduma kwa pamoja kwa taasisi zote zenye huduma zinazoweza kutolewa kwa pamoja;
x. Kuwasilisha Wizara ya Fedha mapendekezo ya mabadiliko ya viwango vya kodi, ushuru na tozo mara baada ya tangazo la kupokea mapendekezo ya mabadiliko ya mfumo wa kodi kutolewa kwa wadau;
xi. Kurasimisha shughuli za kiuchumi ili kuongeza idadi ya walipakodi na wigo wa ukusanyaji wa mapato;

xii. Kutoingia mikataba na wazabuni, wakandarasi na watoa huduma wasiotumia mashine za kielektroniki;

xiii. Kuimarisha usimamizi wa vituo vya makusanyo hususan katika maeneo ya mipaka, viwanja vya ndege, bandari pamoja na vituo vya ukaguzi kwa lengo la kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

xiv. Kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina kwa wakati;

xv. Kuimarisha mifumo ya usimamizi katika Mashirika, Taasisi za Umma, Wakala wa Serikali, na Kampuni ambazo Serikali ina hisa kwa lengo la kuongeza ufanisi; na

xvi. Kuanzisha na kuwekeza katika miradi ya kimkakati kwa lengo la kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

### 4.2.3 Kiwango cha Ubadilishaji Fedha

40. Wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutumia kiwango elekezi cha ubadilishaji wa fedha za kigeni ambacho ni dola moja ya Marekani kwa shilingi za Tanzania 2,555.00.

### 4.2.4 Maombi ya Bajeti ya Nyongeza

41. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25 hakutakuwa na bajeti ya nyongeza ambayo itatengwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za fungu ambazo hazikutengewa bajeti.

### 4.2.5 Uibuaji wa Miradi Mipya

42. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutoa kipaumbele katika kutenga bajeti ya kukamilisha miradi inayoendelea kabla ya kuibua miradi mipya.

#### 4.2.6 Bajeti ya Mishahara

43. Wakati wa maandalizi ya ikama na bajeti ya mishahara kwa mwaka 2024/25, Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

i. Kutenga bajeti ya upandishaji vyeo, ajira mpya, nyongeza ya mshahara ya mwaka, ubadilishaji kada/kazi na uteuzi kwa kuzingatia Mwongozo Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu Uandaaji wa Ikama na Makadirio ya Bajeti ya Mishahara kwa Mwaka 2024/25;

ii. Kuzingatia Mpango wa Rasilimaliwatu wakati wa utengaji wa bajeti ya mishahara ili kuwa na msawazo wa watumishi katika Utumishi wa Umma;

iii. Mafungu yanayolipa mishahara kwa makusanyo ya ndani na yale yanayopelekewa fedha kwa ajili ya mishahara yanapaswa kuhakikisha michango ya kisheria ya watumishi inatengwa na kupelekwa kwa wakati na kwa kiwango sahihi katika mifuko husika ili kuepuka tozo inayotokana na ucheleweshaji wa michango hiyo na usumbufu kwa watumishi pindi wanapostaafu;

iv. Kuandaa bajeti ya mishahara kwa kuzingatia Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 3 wa Mwaka 2022 na Nyaraka za Msajili wa Hazina Na. 3, 4, 5, 6, 7, 8 na 9 za Mwaka 2022 kuhusu Marekebisho ya Mishahara kwa Watumishi wa Umma na Taasisi za Serikali; na

v. Kuzingatia Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2021 kuhusu Matumizi ya Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimaliwatu na Mishahara (HCMIS).

#### 4.2.7 Bajeti ya Matumizi Mengineyo

44. Wakati wa maandalizi ya makadirio ya bajeti ya matumizi mengineyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

i. Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

ii. Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia shughuli za usimamizi wa vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti;
iii. Kutenga bajeti kwa kuzingatia mabadiliko ya miundo ya mipya;
iv. Kutenga bajeti ya kugharamia shughuli za uendeshaji wa ofisi na kulipa stahili za kisheria kwa watumishi (posho za kujikimu, uhamisho, stahili za viongozi, likizo) ili kuepuka uzalishaji wa madeni; na
v. Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi ikijumuisha mafunzo ya matumizi ya mifumo ya usimamizi wa fedha za umma (bajeti, ununuzi na uhasibu) pamoja na usimamizi wa utendaji na rasilimaliwatu.

#### 4.2.8 Bajeti ya Maendeleo

45. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo kwa kuzingatia yafuatayo:

i. Kuwasilisha Wizara ya Fedha takwimu za miadi ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo wiki ya kwanza ya Disemba, 2023 ili kukamilisha maandalizi ya ukomo wa bajeti za mafungu;
ii. Wizara za Kisekta kutojumuisha bajeti za shughuli za mafungu ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye mafungu yao kwa kazi zinazotekelezwa na mafungu hayo. Aidha, Wizara za Kisekta ziwasilishe Wizara ya Fedha wiki ya kwanza ya Disemba, 2023 mchanganuo wa shughuli na bajeti zinazotekelezwa kwenye mafungu mengine ili kujumuishwa kwenye ukomo wa bajeti wa mafungu husika;
iii. Kuzingatia Mwongozo wa Uwekezaji katika Miradi ya Umma uliotolewa mwaka 2022;
iv. Kuzingatia Mwongozo wa Uandaaji Miradi na Majadiliano ya Mikopo, Dhamana na Upokeaji wa Misaada wa mwaka 2020;
v. Kuzingatia Kifungu cha 6 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura 148 kuhusu utaratibu wa kutoa msamaha wa VAT kwa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo;

vi. Kuzingatia Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 kinachoelekeza kutoingia mikataba ya makubaliano na Washirika wa Maendeleo ya kupokea misaada na mikopo pasipo idhini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha;
vii. Kutenga mchango wa Serikali (counterpart fund) katika miradi ya maendeleo yenye masharti hayo inayotekelezwa kwa ushirikiano na Washirika wa Maendeleo;
viii. Kuhakikisha shughuli za Programu zote za Maboresho katika Sekta ya Umma (Usimamizi wa Fedha za Umma, Sekta ya Kilimo, Utumishi wa Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sheria, Mazingira ya Biashara na Uwekezaji na Ardhi) zinajumuishwa (mainstreamed) katika mpango na bajeti;
ix. Kutenga bajeti ya kugharamia fidia katika maeneo yanayotwaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi;
x. Kutumia njia mbadala (Alternative Project Financing) kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo yenye lengo la kuongeza mapato (hati fungani, mikopo n.k);
xi. Kutekeleza miradi yenye mvuto wa kibiashara kwa utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi (PPP) ili kupunguza gharama zinazoweza kuepuka msukumo wa matumizi katika bajeti ya Serikali;
xii. Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 kwa kuweka ukomo wa zabuni zinazoweza kutolewa kwa wasio wazawa ili kuwawezesha wazawa (local content) na kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi. Aidha, kuhakikisha makubaliano yote (Financing Agreement) na Washirika wa Maendeleo yanazingatia ushirikishaji wa wazawa usiopungua asilimia 30 ya gharama ya mradi;
xiii. Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia shughuli za utafiti na maendeleo kwa kutumia mapato ya ndani ya taasisi na ruzuku kutoka Serikali Kuu;
xiv. Kutenga bajeti kwa ajili ya upimaji na upatikanaji wa hati miliki ya maeneo yanayomilikiwa na taasisi za umma; na

xv. Kuzingatia maswala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na masuala ya jamii katika upangaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo.

#### 4.2.9 Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni

46. Katika kutekeleza mkakati wa kuongeza fedha za kigeni, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuendelea:

i. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Fedha za Kigeni, Sura 271 na Kanuni zake kwa lengo la kudhibiti matumizi holela ya fedha za kigeni;
ii. Kutekeleza mikakati ya kisekta ya kuongeza fedha za kigeni na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za kigeni;
iii. Kuweka mazingira rafiki kwa watanzania waliopo nje ya nchi kuwekeza na kutuma fedha za kigeni nchini;
iv. Kuweka mazingira wezeshi ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa ajili ya kukidhi soko la ndani na nje ya nchi;
v. Kutangaza vivutio vya utalii na kuboresha mazingira ya utalii ili kuvutia utalii nchini kwa lengo la kuongeza fedha za kigeni;
vi. Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia mitaji kutoka nje ya nchi; na
vii. Kuhakikisha mikataba mipya inayoingiwa inatumia shilingi ya Tanzania kwa lengo la kupunguza uhitaji wa matumizi ya fedha za kigeni yasiyo ya lazima.
viii. Kutoa kipaumbele kwa bidhaa na huduma za ndani ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni, kuimarisha soko la ndani, kulinda viwanda vya ndani na kuongeza ajira.

#### 4.2.10 Mikakati ya Kulipa na Kudhibiti Ulimbikizaji wa Madeni

47. Katika kudhibiti uzalishaji na ulimbikizaji wa madeni, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia Kifungu cha 52 (1-2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na maelekezo ya *Treasury Circular No. 2 of 2022/23 on Government Domestic Expenditure Arrears and Other Outstanding Obligations* kwa lengo la

kuendelea kusimamia na kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti na Kuzuia Malimbikizo ya Madeni. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia:

i. Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia ulipaji wa madeni kwa kuzingatia miongozo na Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348;
ii. Ulipaji wa madeni uzingatie umri wa madeni pamoja na kutoa kipaumbele kwenye madeni yenye riba na adhabu (penalties); na
iii. Kuhakikisha madai yanayotokana na bidhaa au huduma katika mwaka wa utekelezaji wa bajeti yanalipwa kwa wakati na kiasi stahiki kwa kutumia fedha za migao ya kila mwezi ili kuepuka uzalishaji wa madeni.

#### 4.2.11 Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma

48. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kusimamia nidhamu na uwajibikaji wa matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia yafuatayo:

i. Kuhakikisha kuwa fedha zote zinazopokelewa/zinazokusanywa zinatumika kwa wakati kwa mujibu wa mpango ili kuepuka fedha hizo kuvuka mwaka;
ii. Kuzingatia Mwongozo Kuhusu Maombi na Utoaji wa Fedha za Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali wa mwaka 2021 unaosisitiza kutoingia mikataba bila kuwa na bajeti ya shughuli husika;
iii. Kuhakikisha ushirikishwaji wa taasisi za kisekta unazingatiwa wakati wa upangaji na utekelezaji wa miradi;
iv. Kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani pamoja na ufuatiliaji na tathmini ili kudhibiti matumizi ya fedha za umma;
v. Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi pamoja na kuzingatia bei ya soko wakati wa ununuzi; na
vi. Kuzingatia Mwongozo wa Matumizi ya *Force Account* wa mwaka 2020 katika utekelezaji wa miradi ili kupunguza gharama.

### 4.3 Maelekezo Mahsusi kwa Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma

49. Maafisa Masuuli wa Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa yafuatayo:

i. Kuhakikisha mifuko ya hifadhi ya jamii inakuwa na taarifa sahihi za wanachama ili kuondoa usumbufu wakati wa kustaafu au kumaliza mikataba;
ii. Kuhakikisha taasisi za kibiashara na za kimkakati zinazingatia Waraka wa Msajili wa Hazina Na.1 wa mwaka 2023, katika kuimarisha mfumo wa usimamizi na utendaji kazi;
iii. Kuhakikisha taasisi zinatenga michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi ya Taasisi na asilimia 70 ya ziada ya mapato baada ya kutoa matumizi yaliyoidhinishwa inawasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa kuzingatia Kifungu Na. 8(1)(f) na Kifungu Na. 10(2) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura 370;
iv. Kuhakikisha Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma yanayofanya biashara ambayo hayajaandaa Mipango ya Biashara na Sera ya Gawio (Business Plan and Dividend Policy) wanandaa na kuwasilisha Ofisi ya Msajili wa Hazina;
v. Kuhakikisha makubaliano yanayoingiwa kwenye Mikataba ya Utendaji Kazi yanatekelezwa na taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka zinawasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kuzingatia ratiba ya uwasilishaji wa taarifa hizo;
vi. Kufanya tathmini ya utendaji wa Bodi za Wakurugenzi na taarifa kuwasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina; na
vii. Kuhakikisha maombi ya kuvuka mwaka na fedha yanawasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina na zinatumika kwa malengo yaliyopangwa awali kulingana na sheria na kanuni. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina inapaswa kuwasilisha Wizara ya Fedha maombi ya kuvuka mwaka na fedha kwa kuzingatia Kifungu Na. 29 (2-3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439.

## 4.4 Maelekezo kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

50. Wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2024/25, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutumia ruzuku ya Serikali na mapato ya ndani ya Halmashauri kuzingatia yafuatayo:

i. Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kusimamia na kudumisha masuala ya Ulinzi na Usalama ikiwemo kugharamia vikao vya Kamati ya Usalama ngazi ya Mkoa, Wilaya na Vikao vya Kisheria katika Halmashauri, Tarafa, Kata na Kijiji/Mtaa;
ii. Kutenga bajeti ya kugharamia shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024;
iii. Kutenga bajeti kwa ajili ya kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Tarafa, Kata, Vijiji/Mitaa, Vitongoji na maeneo ya hifadhi kwa lengo la kuboresha matumizi bora ya ardhi;
iv. Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia: ununuzi wa samani; ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa ofisi na makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata na Vijiji/Mitaa;
v. Kutenga bajeti kwa ajili ya shughuli za mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara pamoja na kuhuisha Wasifu wa Uwekezaji wa Mkoa na Halmashauri;
vi. Kutenga bajeti kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi za tarafa, kata, vijijiji na mitaa;
vii. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na kutoa taarifa kila nusu mwaka kwa OR-TAMISEMI;
viii. Kusimamia utekelezaji wa matumizi ya mwongozo wa Special Purpose Vehicle (SPV) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi wa miradi ya kimkakati ili kuongeza mapato ya Halmashauri;
ix. Kushirikisha sekta binafsi katika miradi yenye mwelekeo wa kibiashara ili kuipunguzia Serikali gharama;

x. Kuhakikisha kunakuwa na ratiba ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua na kutoa taarifa kwa OR-TAMISEMI kabla au tarehe 10 ya mwezi unaofuata;
xi. Kutenga bajeti kwa ajili ya kujikinga dhidi ya majanga pamoja na maafa mbalimbali ikiwemo moto, mafuriko na mlipuko wa magonjwa;
xii. Kutumia mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathimini (Intergrated Monitoring and Evaluation System- iMES) katika shughuli za miradi na maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;
xiii. Kutenga bajeti kwa ajili ya kuanza zoezi la tathimini kwa lengo la ukusanyaji wa kodi ya majengo;
xiv. Kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya polisi katika Kata; na
xv. Mamlaka za Serikali za Mitaa zishirikishe Taasisi zilizopo kwenye maeneo yao namna ya kushiriki katika Mpango wa Wajibu wa Makampuni katika Jamii (Corporate Social Responsibility- CSR).

#### 4.4.1 Maelekezo Mahsusi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

i. Kuhakikisha makadirio ya mapato na matumizi ya vituo vya kutolea huduma pamoja na Vijiji/Mitaa na Kata yanaandaliwa na kujumuishwa kwenye Mpango na Bajeti ya Halmashauri;
ii. Kuweka miundombinu wezeshi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya matumizi ya Serikali Mtandao;
iii. Kutenga kiasi kisichopungua asilimia 70 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha asilimia 10 ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na asilimia 10 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazosimamiwa na TARURA kwa Halmashauri zinazokusanya mapato yasiyolindwa ya shilingi bilioni 20 au zaidi;
iv. Kutenga kiasi kisichopungua asilimia 60 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha asilimia 10 ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na asilimia 10 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazosimamiwa na TARURA kwa Halmashauri zinazokusanya mapato yasiyolindwa ya shilingi bilioni 5 au zaidi;

v. Kutenga kiasi kisichopungua asilimia 40 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha asilimia 10 ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa Halmashauri zinazokusanya mapato yasiyolindwa ya kati ya shilingi bilioni 2 hadi shilingi bilioni 5;
vi. Kutenga kiasi kisichopungua asilimia 20 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha asilimia 10 ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa Halmashauri zinazokusanya mapato yasiyolindwa ya chini ya shilingi bilioni 2;
vii. Kutenga kiasi kisichopungua shilingi 200,000 kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi kwa kila Kata/Kijiji/Mtaa kila robo mwaka. Aidha, kwa Halmashauri zinazokusanya mapato chini ya shilingi bilioni 1.5 zinaelekezwa kutenga kiasi kisichopungua shilingi 100,000 kwa Kijiji/Mtaa kila robo mwaka;
viii. Kuendelea kutenga shilingi 100,000 kila mwezi kwa ajili ya posho ya madaraka ya watendaji wa kata;
ix. Kuhakikisha mapato yatokanayo na mazao ya kilimo (asilimia 20), mifugo (asilimia 15) na uvuvi (asilimia 5) yanatengwa na kutumika katika sekta husika kulingana na miongozo iliyopo katika kuboresha sekta hizo na uendelezaji wa mazao ya kimkakati;
x. Kuendelea na usimikaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Tanzania (GoT – HoMIS) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo bado hazijafunga mfumo huo ili kusimamia takwimu za huduma na kudhibiti upotevu wa mapato kwenye vituo vya kutolea huduma za afya;
xi. Kuhakikisha Halmashauri ambazo zimepata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa zinatenga bajeti kutoka kwenye mapato yao ya ndani kwa ajili ya marejesho ya mkopo ; na
xii. Kuhakikisha Halmashauri wanatenga bajeti kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kuchangia Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kulingana na Sheria a Serikali za Mitaa, Sura 290.

### 4.4.2 Maelekezo ya Kisekta katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

i. Kutenga bajeti kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Shule za Msingi na Sekondari kwa kutoa nyenzo za kujifunzia na kufundishia, na kujenga miundombinu rafiki ya elimu;
ii. Kuandaa na kuwasilisha takwimu OR-TAMISEMI kwa ajili ya kuwezesha utengaji wa bajeti ya Elimu Msingi na Sekondari (Kidato cha V na VI) ifikapo tarehe 31 Disemba, 2023;
iii. Kutenga na kuendeleza maeneo ya miundombinu ya kuibua na kuendeleza vipaji na vipawa ikiwemo michezo na sanaa;
iv. Kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na chanjo pamoja na kutenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano ili kuimarisha huduma za lishe;
v. Kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga, kukamilisha na kukarabati miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya;
vi. Kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu ya uhamasishaji kwa wakulima, wafugaji na wavuvi kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kushirikiana na sekta husika;
vii. Kuendelea kutenga bajeti za matengenezo na mafuta ya vyombo vya usafiri kwa Maafisa Ugani, Watendaji wa Kata ili kuwezesha ufuatiliaji wa shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na shughuli nyingine za Serikali katika Kata;
viii. Kuendelea kuwekeza na kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda na kuwawezesha Wajasiriamali wadogo (Wamachinga) kwa kuwapatia elimu ya biashara na ujasiriamali na kuwaunganisha na Taasisi za fedha na masoko;
ix. Kuendeleza mipango miji na matumizi bora ya ardhi hususan miji midogo inayochipukia na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji pamoja na uzingatiaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Uhamasishaji Jamii Ujenzi wa Nyumba Bora wa Mwaka 2019. Aidha, sheria zinazotoa makatozo ya kuvamia maeneo tengefu ikiwemo Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali Maji na Sheria ya Ardhi zizingatiwe kikamilifu; na

x. Kutenga bajeti ya usimamizi na uendelezaji wa maliasili na mazingira.

## 4.5 Masuala Mengine Muhimu ya Kuzingatiwa wakati wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti

51. Pamoja na maelekezo ya ujumla na mahsusi yaliyotolewa, maelekezo mengine yanayopaswa kuzingatiwa ni pamoja na: Masuala ya Muungano; Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa; Masuala ya Watu Wenye Ulemavu; Masuala ya Kijinsia; Mazingira; Afua za Lishe; VVU na UKIMWI; Mapambano Dhidi ya Rushwa; Mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya; Uwekezaji wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi; Uwezeshaji wananchi kiuchumi; na Masuala ya Haki Jinai.

### 4.5.1 Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

52. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 katika uandaaji wa mipango na ugawaji wa rasilimali.

### 4.5.2 Masuala ya Muungano

53. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa:

i. Kuendelea kushughulikia hoja za muungano;
ii. Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia shughuli za ushirikiano na kuimarisha muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ); na
iii. Kuendelea kubadilishana ujuzi katika masuala ya kiuchumi, kimaendeleo na kijamii baina ya SMT na SMZ.

### 4.5.3 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

54. Katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

i. Kuzingatia maelekezo ya Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) wa mwaka 2017/18 - 2024/25 pamoja na mpango kazi wake;

ii. Kuzingatia masuala ya ushirikiano kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa ikijumuisha Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Mashirika ya Kimataifa ili kukuza uwekezaji na kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu;
iii. Kuzingatia masuala ya diplomasia ya uchumi katika uandaaji na utekelezaji wa mpango na bajeti;
iv. Kuwasilisha Wizara ya Fedha makadirio ya michango ya uanachama wa kikanda na kimataifa ndani ya wiki ya kwanza ya Disemba, 2023 kwa ajili ya kujumuishwa kwenye bajeti;
v. Kuhakikisha kuwa sekta zilizoingia makubaliano ya ushirikiano zinatumia kikamilifu fursa zilizopo katika makubaliano husika kwa manufaa ya sekta na taifa kwa ujumla; na
vi. Kuhakikisha viashiria vilivyoainishwa na Washirika wa Maendeleo kama vigezo vya kuipatia nchi msaada wa kibajeti (Budget Support) vinatengewa bajeti ya kuiwezesha nchi kukidhi vigezo vya kupata msaada huo.

#### 4.5.4 Uchumi wa Buluu

55. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuibua fursa zitokanazo na rasilimali za maji bahari na baridi na kuweka mipango na mikakati itakayowezesha fursa hizo kutumika kikamilifu kwa lengo la kuongeza mchango katika mapato ya Serikali, ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

#### 4.5.5 Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

56. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuendelea kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004; matakwa ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010 na maelekezo ya Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu Tanzania wa Mwaka 2022. Aidha, wanaelekezwa kuzingatia Kifungu cha 5.3 cha Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye

Ulemavu wa mwaka 2008 kinachoelekeza kutenga bajeti kwa ajili ya mahitaji ya watumishi wa umma wenye ulemavu.

### 4.5.6 Uandaaji wa Bajeti yenye Mlengo wa Kijinsia

57. Katika uandaaji wa Bajeti yenye mlengo wa Kinjisia (Gender Responsive Budgeting) ambayo inahakikisha kwamba mahitaji na maslahi ya watu kutoka makundi tofauti ya kijamii (jinsia, umri, rangi, na eneo) yanashughulikiwa kupitia sera za matumizi na mapato, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

i. Kutambua masuala ya kijinsia katika maeneo yao kwa kufanya uchambuzi wa kijinsia wa takwimu zilizogawanywa kijinsia ili kutekeleza hatua za kukabiliana na upungufu uliobainika;
ii. Kuchukua hatua za kushughulikia pengo la kijinsia lililobainika katika mpango na bajeti katika taasisi husika;
iii. Kuhakikisha vituo vyote vya kutolea huduma vinafikika na watu wenye ulemavu;
iv. Kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu na huduma stahiki katika vituo maalum kama vile nyumba za wazee na watoto wanaoishi katika mazingira magumu na shule za watoto wenye mahitaji maalum; na
v. Kutenga bajeti kwa ajili ya mafunzo kuhusu uandaaji wa mipango na bajeti yenye mlengo wa kijinsia.

### 4.5.7 Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

58. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na:

i. Kutekeleza Mwongozo wa Biashara ya Kaboni wa Mwaka 2022 ili kuiongezea mapato jamii na Serikali;
ii. Kusimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022- 2032);

iii. Kuhakikisha kuwa maandalizi ya miradi yanajumuisha masuala ya uhifadhi wa mazingira ili kuweza kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kujenga uwezo wa nchi wa kuzuia, kuhimili na kukabiliana wa athari hizo;
iv. Kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa afua mbalimbali za kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi zilizopo katika utekelezaji wa miradi; na
v. Kutenga bajeti kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa hatua mbalimbali za kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika miradi.

### 4.5.8 Afua za Lishe

59. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia utekelezaji wa Mpango wa Pili Jumuishi wa Taifa wa Utekelezaji wa Masuala ya Lishe (NMNAP – II) wa mwaka 2021/22 – 2025/26 kwa lengo la kufikia matokeo tarajiwa ambayo ni:

i. Kuongezeka kwa wigo wa upatikanaji wa huduma za kutosha za lishe zenye ubora na kwa uwiano sawa kwa watu wote katika ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma;
ii. Mabadiliko ya tabia inayosaidia katika kuimarisha hali za lishe miongoni mwa wanawake, wanaume, watoto na vijana balehe;
iii. Kuimarika kwa mifumo endelevu ya chakula inayokidhi mahitaji ya mlaji kilishe;
iv. Kuimarika kwa ushiriki wa wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi katika utekelezaji wa afua za lishe; na
v. Kuimarika kwa mazingira wezeshi yatakayosaidia upatikanaji wa rasilimali watu na fedha zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa afua za lishe.

### 4.5.9 VVU na UKIMWI

60. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

i. Kuendelea kutekeleza matakwa ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa VVU na UKIMWI Sura, 431; na

ii. Kuzingatia Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI na maelekezo ya Mwongozo wa Kudhibiti VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa Mahali pa Kazi Katika Utumishi wa Umma wa Mwaka 2014 kwa lengo la kudhibiti na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kijamii na kiuchumi.

#### 4.5.10 Mapambano Dhidi ya Rushwa

61. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

i. Kutoa kipaumbele kwa kutenga fedha kwa ajili ya kukuza maadili na kupambana na rushwa kwa mujibu wa Mpango na Bajeti wa Muda wa Kati, Sheria ya Kupambana na Rushwa, Sura 329 na Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne 2023/24- 2029/30; na

ii. Kuendelea kushirikiana na Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali katika kukuza maadili na mapambano dhidi ya rushwa.

#### 4.5.11 Mapambano Dhidi ya Dawa za kulevya

62. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

i. Kuendelea kuzingatia matakwa ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura 95 na maelekezo ya Mwongozo wa Utoaji Elimu Kuhusu Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini wa Mwaka 2022; na

ii. Kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa ajili ya kupata uelewa wa kupambana na vita dhidi ya dawa za kulevya.

#### 4.5.12 Uwekezaji wa Ubia kati ya Serikali na Sekta binafsi

63. Maafisa Masuuli wanapaswa kuhakikisha wanatumia njia mbadala hususan Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - PPP kugharamia miradi ya maendeleo yenye sifa ili kupunguza utegemezi kwenye bajeti ya Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi,

Sura 103, Sheria ya Bajeti Sura 439 na Waraka Na. 7 wa Mwaka 2020/21 wa Katibu Mkuu Hazina wenye maelekezo mahususi kuhusu PPP kwa Maafisi Masuuli wote. Ili kufanikisha, pamoja na mambo mengine, Maafisa Masuuli wanapaswa kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya maandalizi ya miradi ya PPP.

#### 4.5.13 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

64. Katika kuwezesha wananchi kiuchumi Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya uratibu wa mazingira wezeshi kwa kutumia fursa za kiuchumi zinazopatikana katika eneo husika ikiwemo fursa za kilimo, mifugo, uvuvi, nishati, madini, biashara, masoko na huduma za kifedha.

#### 4.5.14 Masuala ya Haki Jinai

65. Maafisa masuuli wanaelekezwa kubuni na kutekeleza mikakati ya kusimamia masuala ya Haki Jinai ikiwemo:-

i. Kuwajengea uwezo watumishi wanaounda mnyonyororo wa haki jinai ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa weledi na ufanisi;
ii. Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Mafunzo kwa taasisi za haki jinai ambazo hazina Mpango wa Mafunzo kwa watumishi wake;
iii. Kuweka Mkakati wa Kubaini na Kuzuia Uhalifu kabla Haujatokea kwa kuainisha majukumu ya taasisi mbalimbali za haki jinai na jamii kwa ujumla;
iv. Kuelimisha jamii kuhusu haki za mtuhumiwa pindi anapoingia kwenye mgongano na sheria, masuala ya plea bargaining, haki ya dhamana kwa mtuhumiwa, ukatili wa kijinsia na masuala mengine yote yanayoonekana yanafaa kuelimisha jamii;
v. Kuratibu uanzishwaji wa mifumo inayosomana kama mfumo jumuishi wa haki jinai utakaounganisha taasisi zote za haki jinai utakaosaidia katika kubadilishana taarifa za kiuhalifu na zinazohusiana na hizo;

vi. Kuratibu na kusimamia mchakato wa marekebisho ya sheria zinazotumika kwenye haki jinai ambazo utekelezaji wake unaleta changamoto kwenye baadhi ya maeneo;
vii. Kuimarisha miundombinu ya upatikanaji wa huduma bora kwa watu wenye mahitaji maalum kwenye taasisi za haki jinai; na
viii. Kuratibu uanzishwaji wa mifumo ya TEHAMA katika upelelezi na uendeshaji mashtaka.

### 4.6 Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti

66. Ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti utazingatia Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini na utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa mwaka 2022 na miongozo mingine iliyopo ya kisekta ya ufuatiliaji na tathmini.

#### 4.6.1 Ufuatiliaji na Tathmini

67. Katika kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

i. Kufanya tathmini ya vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi na kuainisha mikakati ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato hayo;
ii. Kuimarisha vitengo vipya vya ufuatiliaji na tathmini kwa kutenga bajeti, watumishi, kuandaa mpango wa kurithisha maarifa kwa watumishi wapya ili viweze kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa;
iii. Kuhakikisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kinafuatilia uzingatiwaji wa Sheria ya Bajeti kuhusu utendaji wa Kamati ya Bajeti kwa lengo la kupitia na kujadili taarifa za ufuatiliaji, tathmini na utekelezaji kila robo mwaka ili kuleta uwajibikaji;
iv. Kuzingatia maelekezo ya Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathimini wa Miradi na Programu za Maendeleo wa Mwaka 2022 uliotolewa na Wizara ya Fedha;

v. Kutenga fedha za kuwezesha ufuatiliaji na tathmini na kuhakikisha kunakuwa na mpango shirikishi kwa kuwajumuisha wadau wote katika ngazi ya Idara/vitengo ndani ya taasisi au taasisi nyingine ili kupunguza gharama na kuongeza ufanisi;

vi. Kuzingatia matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS) kama ilivyoelekezwa kwenye ya Waraka wa Hazina Na. 5 wa Mwaka 2021/22;

vii. Kuweka mifumo thabiti ya ufuatiliaji na tathmini na kuhakikisha kuwa mpango na bajeti unaakisi malengo, shabaha na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26;

viii. Kutenga fedha kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera hususan zilizotekelezwa kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano kwa lengo la kubaini uhitaji wa mabadiliko ya sera; na

ix. Kuandaa viashiria vya kupima utekelezaji wa malengo ya Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili viwe vipimio vya mafanikio ya taasisi husika.

### 4.6.2 Uandaaji na Uwasilishaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti

68. Kwa mujibu wa Kifungu cha 55 cha Sheria ya Bajeti Sura 439, Maafisa Masuuli wanapaswa kuandaa na kuwasilisha Wizara ya Fedha taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka ndani ya siku 30 baada ya kukamilika kwa robo ya mwaka husika. Nakala za taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka mzima kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwasilishwe OR – TAMISEMI, Taasisi na Mashirika ya Umma ziwasilishwe Ofisi ya Msajili wa Hazina, nakala kwa Wizara mama. Aidha, taarifa za utekelezaji za mwaka ziwasilishwe katika nakala mango na tete kabla ya tarehe 15 Oktoba kila mwaka wa fedha.



# VIAMBATISHO VYA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NABAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25



# VIAMBATISHO VYA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NABAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25

**KIAMBATISHO NA. 1**

# VIAMBATISHO VYA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25

**YALIYOMO**


Kiambatisho Na. 1A ........ 1
MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI ........ 1
1.1 Utangulizi ........ 1
1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi ........ 1
1.3 Deni la Serikali ........ 8

Kiambatisho Na. 1B ........ 10
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23 ........ 10
2.1 Utangulizi ........ 10
2.2 Mapato na Matumizi ........ 10
2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2022/23 ........ 11
2.4 Fursa Zilizojitokeza katika Utekelezaji wa Bajeti ........ 20
2.5 Changamoto Zilizojitokeza katika Utekelezaji wa Bajeti ........ 20
2.6 Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti ........ 21
2.7 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2023/24 ........ 21

Kiambatisho Na. 1C ........ 23
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2023/24 ........ 23
3.1 Utangulizi ........ 23
3.2 Sura ya Bajeti ya Mwaka 2023/24 ........ 23
3.3 Utekelezaji wa Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2023/24 ........ 24

Kiambatisho Na. 1D ........ 32
MUUNDO WA UWASILISHAJI WA MTEF 2024/25 - 2026/27 ........ 32

Kiambatisho Na. 1E ........ 33
RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 ........ 33

Kiambatisho Na. 1F ........ 37
MUUNDO WA TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI ........ 37

**Kiambatisho Na. 1A**

**MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI**

## 1.1 Utangulizi

1. Sura hii inaelezea mwenendo wa hali ya uchumi wa dunia, kikanda na Tanzania kwa mwaka 2022 na mwelekeo wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2023 hadi mwaka 2024 na deni la Serikali.

### 1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi

### 1.2.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Kikanda

2. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (International Monetary Fund - IMF) toleo la Oktoba 2023, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.3 mwaka 2021. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imepungua kutokana na athari za janga la UVIKO-19, vita kati ya Urusi na Ukraine pamoja na mabadiliko ya tabianchi. Uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.0 mwaka 2023 na asilimia 2.9 mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 1.1**). Makadirio hayo ni chini ya wastani wa ukuaji wa asilimia 3.8 kwa mwaka katika kipindi cha mwaka 2000 hadi mwaka 2019. Kasi ndogo ya ukuaji imetokana na kupanda kwa viwango vya riba katika nchi zilizoendelea ili kukabiliana na mfumuko wa bei ambao umeendelea kuathiri shughuli za kiuchumi katika nchi mbalimbali.

3. Katika nchi zilizoendelea uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.6 mwaka 2021. Sababu kubwa iliyochangia mwenendo huo ni maamuzi ya kupandisha riba za benki kuu katika nchi zilizoendelea hususan Marekani na baadhi ya nchi za Ulaya kwa lengo la kukabiliana na mfumuko wa bei. Hatua hiyo ilisababisha uhaba wa fedha katika soko la dunia na hivyo kuchangia ongezeko la gharama za mikopo. Katika nchi hizo, ukuaji unatarajiwa kupungua hadi asilimia 1.5 mwaka 2023 na asilimia 1.4 mwaka 2024.


4. Kwa upande wa nchi zinazoibukia na zinazoendelea, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2021. Hii ilitokana na athari za janga la UVIKO-19 pamoja na kuzorota kwa soko la bidhaa nchini China na vita vya Urusi na Ukraine. Aidha, mwaka 2023 ukuaji unatarajiwa kuwa asilimia 4.0 sawa na ukuaji unaotarajiwa mwaka 2024.

5. Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi ulishuka kutoka asilimia 4.7 mwaka 2021 hadi asilimia 4.0 mwaka 2022. Kushuka kwa kasi ya ukuaji ulitokana na uhaba wa fedha ulioambatana na mabadiliko hasi katika masharti ya biashara (*negative shift in the commodity term of trade*). Mwaka 2023, ukuaji unatarajiwa kuwa asilimia 3.3 na kuongezeka hadi asilimia

4.0 mwaka 2024. Maoteo hayo yanatokana na kudorora kwa uchumi wa mataifa makubwa katika ukanda huo ikiwa ni pamoja na Afrika Kusini na Nigeria kutokana uhaba wa usambazaji wa umeme na usalama mdogo katika sekta ya mafuta mtawalia.

6. Kulingana Taarifa ya Benki ya Maendeleo Africa (Africa Development Bank Group) 2023, ukuaji wa uchumi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ulikuwa asilimia 3.16 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.65 mwaka 2021 (**kielelezo No. 1.1**). Kupungua kwa ukuaji kulichangiwa zaidi na kudorora kwa hali ya kifedha duniani, na vita kati ya Nchi za Urusi na Ukraine. Vilevile athari za janga la UVIKO-19 na mabadiliko ya hali ya hewa.

**Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia na Kikanda**




**Tanbihi**: *Maoteo


### 1.2.2 Ukuaji wa uchumi wa Tanzania

7. Pamoja na changamoto zilizojitokeza na kuathiri uchumi wa dunia, uchumi wa Tanzania uliendelea kuimarika kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali. Hatua hizo ni pamoja na utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine ikiwemo utoaji wa ruzuku ya mbolea na mafuta ya petroli. Aidha, sababu nyingine za kuimarika kwa uchumi ni uwekezaji wa kimkakati uliofanywa na Serikali katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli, viwanja vya ndege; na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hususan makaa ya mawe, gesi, mawe ya chokaa na shaba pamoja na shughuli za utalii.

8. Kutokana na jitihada hizo, Pato la Taifa katika mwaka 2022 lilikua kwa asilimia 4.7 na linatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.2 mwaka 2023 na asilimia 5.8 mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 1.2)**. Aidha, Pato la Taifa kwa kipindi

cha Januari hadi Juni 2023 lilikua kwa wastani wa asilimia 5.3 ikilinganishwa na asilimia 5.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.


**Kielelezo Na. 1.2: Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Tanzania**




**Tanbihi**: * Maoteo

9. Katika mwaka 2022, shughuli zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa ni pamoja na: kilimo asilimia 26.2; ujenzi asilimia 14.1; madini asilimia 9.1; biashara asilimia 7.9; viwanda asilimia 7.1 na usafirishaji kwa asilimia 6.7. **Kielelezo Na. 1.3** kinaonesha mchango wa shughuli katika ukuaji wa Pato la Taifa.

**Kielelezo Na. 1.3: Mchango wa Shughuli za kiuchumi katika ukuaji wa Pato la Taifa, Mwaka 2022**



### 1.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia na Kikanda

10. Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (International Monetary Fund - IMF) ya Oktoba 2023, inaonesha kuwa mfumuko wa bei duniani unatarajiwa kushuka kutoka asilimia 8.7 mwaka 2022 hadi asilimia 6.9 mwaka 2023 na unakadiriwa kuwa asilimia 5.8 mwaka 2024. Hali hiyo imechochewa na kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na utekelezaji wa sera ya fedha katika nchi zilizoendelea.

11. Katika mwaka ulioshia Juni 2023, mfumuko wa bei katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) uliongezeka hadi asilimia 14.3 kutoka asilimia 6.3 mwaka ulioishia Juni 2022. Hali hii ilichangiwa zaidi na ongezeko la bei za baadhi ya bidhaa za vyakula.

### 1.2.4 Mfumuko wa Bei Nchini

12. Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.6 mwaka 2022/23, kiwango ambacho kipo ndani ya lengo la nchi na mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC). Aidha, mfumuko wa bei kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2023 ulikuwa wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 4.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 3.0 – 7.0 ambalo linaendana na viwango vya kikanda kutokana na matarajio ya hali nzuri ya hewa, utulivu wa bei za bidhaa katika soko la dunia pamoja na utekelezaji wa sera za fedha.

### 1.2.5 Ujazi wa Fedha na Mikopo

13. Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutekeleza sera ya fedha kulingana na malengo ya kiuchumi yaliyowekwa na Serikali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha utulivu wa mfumuko wa bei na kuimarisha ukuaji wa uchumi. Mwaka 2022/23, Benki Kuu ilitekeleza sera ya fedha iliyolenga kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi kwenye uchumi ili kukabiliana na shinikizo la ongezeko la mfumuko wa bei linalotokana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine, athari za janga la UVIKO-19 na mabadiliko ya tabianchi bila kuathiri kasi ya ukuaji wa uchumi. Utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kuhakikisha uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi kwenye mfumo wa kibenki kinachoendana na mahitaji halisi ya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

14. Katika mwaka 2022/23, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 13.7, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 12.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 na lengo la ukuaji wa asilimia 10.3 kwa mwaka 2022/23. Aidha, wastani wa fedha taslimu ulikua kwa asilimia 12.8 ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 11.4. Ukuaji huu ulikuwa sambamba na mahitaji ya shughuli za kiuchumi.

15. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 22.2 kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na lengo la ukuaji la asilimia 10.7. Ukuaji huo umeongezeka ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.9 mwaka 2021/22. Ukuaji huu unaakisi ongezeko la mahitaji ya mikopo mipya kwa sekta binafsi kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na janga la UVIKO – 19; jitihada zinazoendelea kutekelezwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; na utekelezaji wa sera wezeshi za fedha na bajeti.

16. Katika kipindi cha mwaka 2022/23, mikopo kwa sekta binafsi iliyoelekezwa kwenye shughuli za kilimo ilikua kwa kasi zaidi, hadi kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 44.5 kutoka asilimia 0.3 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Ukuaji huu umetokana na hatua za ziada za kisera zilizochukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu kwa lengo la kuongeza chachu ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi hususan katika shughuli za kilimo kwa riba nafuu, ikiwemo mkopo maalum wa shilingi trilioni moja kwa benki na taasisi za fedha ili kutoa mikopo kwenye sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10. Aidha, sehemu kubwa ya mikopo imeendelea kuelekezwa katika shughuli binafsi (shughuli ndogondogo za kiuchumi) kwa asilimia 38.4, ikifuatiwa na biashara (asilimia 16.1), uzalishaji viwandani (asilimia 10.1) na kilimo asilimia 8.7.

### 1.2.6 Viwango vya Riba

17. Katika kipindi cha mwaka 2022/23, riba ya jumla katika soko la fedha baina ya mabenki iliendelea kuwa tulivu kwa wastani wa asilimia 3.55 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.22 kwa mwaka 2021/22. Aidha, riba ya jumla ya dhamana za muda mfupi za Serikali zilifikia wastani wa asilimia 5.73. Viwango vya riba za mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi vimeendelea kupungua na kufikia wastani wa asilimia 16.04 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.41 mwaka 2021/22. Mwenendo huu ulichagizwa zaidi na hatua za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu katika kupunguza riba za mikopo. Aidha, wastani wa viwango vya jumla vya riba za amana ulifikia asilimia 8.01 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.18 mwaka 2021/22.

### 1.2.7 Viwango vya Ubadilishaji Fedha

18. Katika kipindi cha mwaka 2022/23, thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilipungua kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni kwenye uchumi; kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia; na kupungua kwa fedha za kigeni zinazoingia nchini kutokana na kupanda kwa riba za benki kuu katika nchi zilizoendelea. Hivyo, dola moja ya Marekani katika soko la jumla ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,321.69 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi 2,309.50 mwaka 2021/22. Kupungua kwa thamani ya shilingi kwa chini ya asilimia moja kwa mwaka, kulitokana na uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni nchini sambamba na hatua zilizochukuliwa na

Benki Kuu katika kuongeza utulivu katika soko la jumla la fedha za kigeni. Aidha, katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,428.26 ikilinganishwa na shilingi 2,316.73 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

### 1.2.8 Akiba ya Fedha za Kigeni

19. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi. Hadi kufikia Juni 2023, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani bilioni 5.45 ikilinganishwa na dola bilioni 5.11 Juni 2022. Kiasi hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.9. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi miezi 4.0 na zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### 1.2.9 Sekta ya Benki

#### a) Huduma Jumuishi za Fedha

20. Benki Kuu iliendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kuwa huduma za kifedha zinawafikia wananchi wengi na kwa gharama nafuu ikiwa ni pamoja na kuendelea kutekeleza mradi wa mfumo wa malipo ya papo kwa hapo (TIPS), ambao unalenga kuongeza muingiliano baina ya watoa huduma za fedha nchini. Kwa mujibu wa Utafiti wa Huduma za Fedha wa Mwaka 2023 (Tanzania Finscope Survey, 2023), asilimia ya watu wazima wanaotumia huduma za fedha imeongezeka kutoka asilimia 65 mwaka 2017 hadi asilimia 76 mwaka 2023. Utafiti huo pia ulibainisha kuwa watanzania wengi wanazifikia na kutumia huduma za fedha kupitia simu za mkononi.

#### b) Huduma Ndogo za Fedha

21. Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya uratibu, usajili na uhamasishaji wa uanzishaji na uendelezaji wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha (Community Microfinance Groups). Hadi Juni 2023, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa leseni 1,307 kwa watoa huduma daraja la pili na leseni 801 kwa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo pamoja na kusajili vikundi 42,257 vya kijamii. Aidha, watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili wamekopesha mikopo yenye thamani ya shilingi billioni 915 kwa wajasiriamali wadogo na wa kati nchini.

#### c) Ukwasi na Faida katika Benki za Biashara

22. Sekta ya benki imeendelea kuimarika na kutengeneza faida ikiwa na viwango vya kutosha vya mitaji na ukwasi. Viwango vya amana na rasilimali vimeendelea kuongezeka na hivyo kusaidia sekta ya benki kubaki imara dhidi ya misukosuko kutoka ndani na nje ya nchi. Uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali zote ulifikia asilimia 18.3 Juni 2023, ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika kisheria cha asilimia 10. Aidha, uwiano wa ukwasi (Liquid

Assets to Demand Liabilities) ulikuwa asilimia 25.1 Juni 2023 juu ya kiwango kinachokubalika kisheria cha angalau asilimia 20 na hivyo kuendelea kuwa toshelevu kwa mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Sekta ya benki imeendelea kutengeneza faida ambapo faida baada ya kodi kwa miezi sita ya kwanza ya mwaka 2023 iliongezeka kufikia shilingi bilioni 744.8 kutoka shilingi bilioni 562.8 katika miezi sita ya kwanza ya mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 32.3.

d) **Mikopo Chechefu**

23. Ubora wa rasilimali za benki umeendelea kuimarika kutokana na kupungua kwa kiwango cha mikopo chechefu hadi wastani wa asilimia 5.3 Juni 2023 kutoka asilimia 7.8 Juni 2022. Hali hii ilichangiwa zaidi na hatua zilizochukuliwa na Serikali ikiwemo kuboresha mazingira ya kufanya biashara, kulipa malimbikizo ya madai na kusimamia ukwasi katika uchumi, hali iliyowezesha wateja kulipa mikopo kwa wakati. Hatua nyingine zilizochukuliwa na Benki Kuu ni pamoja na: kuhimiza benki za biashara kuongeza umakini katika kuchakata maombi ya mikopo; kuwaondoa katika sekta ya benki wafanyakazi wasio waaminifu; kuamuru benki kutumia taarifa za mikopo kutoka katika kanzidata ya taarifa za wakopaji; utekelezaji wa kanuni za kuwalinda watumiaji wa huduma za kibenki kwa kuhakikisha utunzaji wa haki na usawa kwa wateja; na kuhakikisha uwepo wa uwazi wa taarifa za kifedha kwa kutoa elimu ya fedha kwa watumiaji wa huduma za kifedha. Vilevile, Benki Kuu ilielekeza benki na taasisi za fedha kuwa na mifumo ya udhibiti na utawala bora kwa kupitia upya mifumo iliyopo ili kukidhi mabadiliko na maendeleo katika sekta ya benki.

### 1.2.10 Sekta ya Nje

24. Sekta ya Nje imeendelea kukabiliwa na athari za mwenendo usioridhisha wa uchumi wa dunia uliosababishwa na vita kati ya Urusi na Ukraine, madhara ya janga la UVIKO-19 na mabadiliko ya tabianchi. Hali hii imesababisha kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi wa bidhaa na huduma duniani na hivyo kusababisha kupanda kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali katika soko la dunia.

**a) Urari wa Malipo ya Kawaida**

25. Urari wa malipo ya nje ulifikia nakisi ya dola za Marekani milioni 4,860.1 mwaka 2022/23. Aidha, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 16.3 hadi dola za Marekani milioni 12,796.0, kufuatia ongezeko la mapato ya usafirishaji, madini na bidhaa za viwandani. Wakati huohuo, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 24 kufikia dola za Marekani milioni 17,007.2 kutokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa hususan mafuta kufuatia kupanda kwa bei katika soko la dunia.

**b) Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa na Huduma**

**28.** Mwaka 2022/23, urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 4,211.2, kutokana na ongezeko la gharama za uagizaji wa bidhaa. Aidha, urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 7,100.3. Vilevile, urari wa wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,889.1, kutokana na kuimarika kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii na usafirishaji kulikosababishwa na kupungua kwa athari za UVIKO-19 pamoja na juhudi za Serikali katika kuvutia watalii kutoka nchi mbalimbali duniani.

## 1.3 Deni la Serikali

26. Hadi Juni 2023, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 82,137.9 kati ya deni lote, deni la nje ni shilingi bilioni 53,211.53 na deni la ndani ni shilingi bilioni 28,926.37. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba 2022 inaonesha kuwa viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda wa kati na mrefu kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.3**.

**Jedwali Na. 1.3 Tathmini ya Uhimilivu wa Deni**

| Viashiria Vya Uhimilivu | Ukomo | 21/22 | 22/23 | 23/24 | 24/25 | 25/26 | 26/27 | 27/28 | 32/33 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni la Nje | | | | | | | | | |
| Uwiano wa thamani ya sasa ya Deni kwa Pato la Taifa | 40 | 18.1 | 17.7 | 17.3 | 16.4 | 15.8 | 15.8 | 16.3 | 15.4 |
| Uwiano wa thamani ya sasa ya Deni kwa Mauzo ya Nje ya Nchi | 180 | 119.6 | 113.4 | 108.1 | 104.0 | 101.9 | 101.3 | 99.7 | 92.1 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mauzo ya Nje ya Nchi | 15 | 13.5 | 14.1 | 9.6 | 8.9 | 8.5 | 8.2 | 8.8 | 10.6 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | 18 | 14.1 | 14.9 | 10.4 | 9.6 | 9.3 | 9.3 | 10.9 | 12.2 |
| Deni la Serikali (Ndani na Nje) | | | | | | | | | |
| Uwiano wa Thamani ya sasa ya Deni kwa pato la Taifa | 55 | 32.5 | 31.9 | 30.9 | 29.5 | 28.4 | 27.8 | 28.6 | 30.8 |
| Uwiano wa Thamani ya sasa ya Deni kwa Mapato | N/A | 217 | 207 | 202 | 196 | 194 | 195 | 207.7 | 207.1 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | N/A | 34.0 | 41.6 | 33.3 | 30.5 | 27.6 | 27.7 | 30.1 | 41.0 |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

### 1.3.1 Tathmini ya Uwezo wa Nchi Kukopesheka

27. Tathmini ya uwezo wa nchi kukopesheka (Credit Rating) ilikamilika mwaka 2022/23 ambapo kampuni za Moody's Investors Service Ltd na Fitch

Rating Services Ltd zilichapisha matokeo ya daraja B2+ na B+ mtawalia. Alama hizo zinabainisha kuwa mwelekeo wa hali ya uchumi, usimamizi wa deni, uwekezaji na hali ya kisiasa nchini ni ya kuridhisha. Matokeo haya yanatokana na kuwepo kwa utulivu wa kisiasa nchini na hatua ya Serikali ya awamu ya sita katika kufungua uchumi. Tathmini hii itaiwezesha nchi kutambulika zaidi katika masoko ya fedha ya kimataifa na hivyo kuongeza sifa za kuvutia uwekezaji na kupanua wigo wa kupata mikopo kwa Serikali na sekta binafsi. Aidha, Serikali itaendeleza usimamizi madhubuti wa hali ya uchumi, kuimarisha uhimilivu wa deni la Serikali, kuvutia uwekezaji na kuboresha hali ya kisiasa.

**Kiambatisho Na. 1B**

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23

### 2.1 Utangulizi

28. Kiambatisho hiki kinaelezea muhtasari wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23. Mapitio hayo yamefanyika katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali kwa kuzingatia malengo na shabaha za bajeti. Maelezo ya kina yanapatikana katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2024/25.

### 2.2 Mapato na Matumizi

29. Katika mwaka 2022/23, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia shilingi bilioni 41,480.6. Hadi Juni 2023, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 38,977.0 sawa na asilimia 94.0 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 26,277.9 mapato ya ndani sawa na asilimia 93.8 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 28,017.9; shilingi bilioni 3,562.9 ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 76.6 ya lengo la shilingi bilioni 4,648.6; na shilingi bilioni 9,136.2. ni mikopo ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi sawa na asilimia 103.7 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 8,814.2. Aidha, Serikali imetumia shilingi bilioni 40,853.3 kugharamia utekelezaji wa shughuli na miradi mbalimbali ya Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 26,882.6 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 13,970.7 ni matumizi ya maendeleo. Tofauti ya mapato na ridhaa ya matumizi iliyotolewa ya shilingi bilioni 1,876.3 iligharamiwa na mkopo wa muda mfupi. **Jedwali Na. 2.1** linaonesha mchanganuo wa makadirio ya mapato na matumizi pamoja na ufanisi katika eneo la mapato na matumizi.

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2022/23 (Shilingi Milioni)**

| | Bajeti | Halisi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **Mapato ya Ndani** | **28,017,867** | **26,277,887** | 93.8% |
| Mapato ya Kodi na Yasiyo ya Kodi (TRA) | 23,652,758 | 22,610,162 | 95.6% |
| Mapato Yasiyo ya Kodi (MDAs) | 3,352,824 | 2,646,686 | 78.9% |
| Mapato ya Halmashauri | 1,012,286 | 1,021,039 | 100.9% |
| **Misaada** | **1,101,489** | **596,380** | 54.1% |
| **Mikopo Nafuu** | **3,547,072** | **2,966,481** | 83.6% |
| **Mikopo ya Kibiashara Kutoka Nje** | **3,034,004** | **3,011,725** | 99.3% |
| **Mikopo ya Kibiashara Kutoka Ndani** | **5,780,148** | **6,124,512** | 106.0% |
| Mikopo ya Kugharamia Miradi | 2,480,148 | 2,610,598 | 105.3% |
| Mikopo ya Kulipa Mtaji Deni la Ndani | 3,300,000 | 3,513,914 | 106.5% |
| **JUMLA YA MAPATO** | **41,480,580** | **38,976,986** | **94.0%** |
| | | | |
| **Matumizi ya Kawaida** | **26,474,576** | **26,882,592** | 101.5% |
| Mishahara | 9,830,753 | 9,046,205 | 92.0% |
| Mfuko Mkuu wa Serikali (Deni & CFS Others | 11,308,362 | 11,951,425 | 105.7% |
| Matumizi Mengineyo | 5,335,461 | 5,884,961 | 110.3% |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **15,006,002** | **13,970,706** | 93.1% |
| Miradi ya Fedha za Ndani | 12,306,921 | 12,259,082 | 99.6% |
| Miradi ya Fedha za Nje | 2,699,081 | 1,711,624 | 63.4% |
| **JUMLA MATUMIZI** | **41,480,578** | **40,853,298** | **98.5%** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

## 2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2022/23

30. Utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23 umekuwa na mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali kama ifuatavyo:

### a) Sekta ya Uchukuzi

31. Utekelezaji wa miradi katika Sekta ya Uchukuzi uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 2,041.2 ambapo shilingi bilioni 2,308.3 zilitolewa sawa na asilimia 113.1. Baadhi ya miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa katika sekta hii ni pamoja na:

i. **Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa *(SGR):*** Mradi wa ujenzi wa reli ya *SGR* upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo: Dar es Salaam – Morogoro (km 300) asilimia 98.48; Morogoro – Makutupora (km 422) asilimia 94.74; Mwanza - Isaka (km 341) asilimia 37.20; Makutupora - Tabora (km 371) asilimia 10.12; Tabora - Isaka (km 165) asilimia 4.10; na Tabora – Kigoma (Km 506) asilimia 0.29;

ii. **Kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania:** Serikali ilikamilisha ununuzi wa ndege moja (1) ya mizigo aina ya Boeing 767-300F. Aidha, sehemu ya malipo ya ndege tatu (3) aina ya Boeing 737-9 Max (2) na Boeing 787- 8 Dreamliner (1) pamoja na malipo ya awali ya ununuzi wa ndege moja (1) aina ya Boeing Business Jet 737-7 yalifanyika;

iii. **Kuendelea na uboreshaji wa huduma katika viwanja vya ndege** kwa kununua mitambo ya mawasiliano ya sauti kati ya marubani na waongoza ndege na kufanya usimikaji na majaribio katika viwanja 12 vya ndege vya JNIA, KIA, Abeid Aman Karume International Airport (Zanzibar), Tanga, Arusha, Pemba, Mtwara, Dodoma, Mwanza, Tabora, Kigoma na Songwe; na

iv. **Ujenzi na ukarabati wa meli:** Serikali imeendelea na ujenzi wa Meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu ambao umefikia asilimia 85; ukarabati wa meli ya MV Umoja (asilimia 95) na MT Sangara (asilimia 90.7).

**b) Sekta ya Nishati**

32. Utekelezaji wa miradi katika sekta ya nishati uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 2,676.2 kwa mwaka 2022/23 ambapo shilingi bilioni 2,225.8 zilitolewa sawa na asilimia 83.2. Miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa katika sekta hii ni pamoja na: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - JNHPP (MW 2,115) ambao umefikia asilimia 91.72; ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Rufiji – Chalinze (asilimia 98) na Kituo cha Kupoza Umeme Chalinze (asilimia 80.5); Usambazaji wa Umeme Vijijini umewezesha Vijiji 10,753 kati ya Vijiji 12,318 sawa na asilimia 87.3 kuunganishiwa umeme; kukamilika kwa asilimia 100 kwa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension (MW 185); na utekelezaji wa Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga (asilimia 98.5).

33. Serikali iliendelea pia na maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Liquiefied Natural Gas - LNG) ambapo majadiliano ya Mkataba wa Nchi Hodhi (Host Government Agreement–HGA) na Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (Amended Production Sharing Agreement–PSA) baina ya Serikali na wawekezaji yalikamilika; kuendelea na malipo ya fidia na ununuzi wa hisa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani, Tanga (Tanzania), (East African Crude Oil Pipeline – EACOP); na usambazaji wa Gesi Asilia Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani kwa ajili ya matumizi ya majumbani, kwenye viwanda, taasisi na magari.

**c) Sekta ya Ujenzi**

34. Utekelezaji wa miradi katika sekta ya ujenzi iliidhinishiwa shilingi bilioni 2,169.6 ambapo shilingi bilioni 2,207.1 zilitolewa sawa na asilimia 101.7. Miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa katika sekta hii ni pamoja na:

i. **Ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja:** Jumla ya km 1,178.43 za barabara kuu na barabara za Mikoa zimejengwa. Kati ya hizo km 297.97 ni barabara za lami na km 880.46 ni barabara za changarawe. Aidha, jumla ya km 22,873.47 za barabara za vijijini na mijini zimekamilika ambapo kati ya hizo km 204.17 ni barabara za lami. Kwa upande wa madaraja, Serikali imekamilisha Daraja Jipya la Wami na kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kigongo Busisi ambao umefikia asilimia 78;

ii. **Ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege na vivuko:** Serikali imekamilisha ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Songea na Mtwara (awamu I) na ujenzi wa viwanja vingine vya Songwe (asilimia 98), Iringa (asilimia 70), Musoma (asilimia 50), Msalato - Package *1* - miundombinu (asilimia 34.72) na Msalato - *Package 2* - majengo (asilimia 6.15) unaendelea. Aidha, miradi ya vivuko iliyotekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa ukarabati wa vivuko sita (6) na kuendelea na ujenzi wa vivuko sita (6); na

iii. **Miradi mingine ya ujenzi**: Ujenzi wa miundombinu ya kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na majiji mengine ambapo barabara ya njia nane (8) Kimara – Kibaha imekamilika; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maegesho; na ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali ambapo Magomeni Kota awamu ya pili Block A imekamilika.

**d) Sekta ya Kilimo**

35. Utekelezaji wa miradi katika sekta ya kilimo iliidhinishiwa shilingi bilioni 631.4 ambapo shilingi bilioni 501.9 zilitolewa sawa na asilimia 79.5. Sekta ya kilimo inahusisha sekta ndogo za kilimo (mazao), mifugo na uvuvi. Shughuli za vipaumbele zilizotekelezwa kwa upande wa Sekta ya Kilimo (mazao) ni pamoja na:

i. **Uzalishaji wa mazao ya kilimo:** uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2022/23 ni tani 20,402,014 ikilinganishwa na mahitaji ya chakula tani 16,390,404 mwaka 2023/24 hivyo nchi imezalisha ziada ya tani 4,011,610 sawa na utoshelevu asilimia 124. Mafanikio haya yametokana na kutolewa na kusambazwa kwa mbolea ya ruzuku tani 531,091 kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini na uwepo wa mvua za kutosha katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, uzalishaji wa mazao yenye asilili ya biashara yalifikia tani 1,097,115 ikilinganishwa na tani 973,436 mwaka 2021/22 na mazao ya bustani yalifikia tani 7,723,115.66 ikilinganishwa na tani 7,304,723 mwaka 2021/22; na

ii. **Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (Building a Better Tomorrow - BBT)**: Wizara ya Kilimo imeanzisha Programu ya BBT kwa ajili ya kuongeza ajira za vijana na wanawake 1,000,000 kwenye Sekta ya Kilimo ifikapo mwaka 2025. Hatua iliyofikiwa ni: Kubainisha na kupima kwa ajili ya kuyapatia hati miliki mashamba makubwa ya pamoja 28 yenye ukubwa wa ekari 196,889 katika mikoa ya Dodoma (ekari 34,613), Kagera (ekari 5,640), Mbeya (ekari 52,165), Njombe (ekari 87,501), Kigoma (ekari 14,875) na Pwani (ekari 2,095); na kutoa mafunzo ya kilimo kwa vijana 812 na kuanza mafunzo ya uzalendo katika kambi ya JKT.

iii. **Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji:** Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kuanza ujenzi wa skimu mpya 19 na kukarabati skimu 19 ambazo zikikamilika zitaongeza eneo la umwagiliaji kwa jumla ya hekta 95,000 na hivyo kufanya eneo la kilimo linalomwagiliwa kuwa hekta 822,285.6; kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 1,604 za mashamba ya utafiti na uzalishaji wa mbegu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30; kuanza ujenzi wa mabwawa 10 yenye jumla ya mita za ujazo 131,535,000; kuanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mabonde 22 ya kimkakati yenye jumla ya hekta 306,361; kununuliwa kwa mitambo 15 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji. Aidha, utekelezaji wa miradi hiyo imezalisha jumla ya ajira kwa watu wapatao 298,635 katika maeneo ya miradi hiyo.

**e) Mifugo**

36. Utekelezaji wa miradi katika Sekta ndogo ya Mifugo uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 46.7 ambapo shilingi bilioni 29.7 zilitolewa sawa na asilimia 64.0. Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi katika Sekta ndogo ya Mifugo ambapo miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa katika sekta hii ni pamoja na:

i. **Kuimarisha afya ya mifugo:** Hatua iliyofikiwa ni: ujenzi wa majosho 257 katika Mikoa 25 ambapo 246 yamekamilika na ujenzi wa majosho 11 unaendelea; kununuliwa kwa lita 52,560 za dawa ya kuogesha mifugo na kusambazwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 172 na mashamba matano (5) ya kuzalisha mitamba; kusambazwa kwa chanjo za mifugo dozi 696,393,500 dhidi ya magonjwa mbalimbali ya kipaumbele kati ya dozi 552,000,000 zilizopangwa; na kununuliwa kwa gari lenye mfumo baridi kwa ajili ya kusambaza chanjo; na

ii. **Uboreshaji wa mbari kwa ajili ya uzalishaji wa maziwa na nyama:** Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa ng'ombe wazazi 1,230 na kusambazwa katika Mashamba ya Serikali; Kuzalisha mitamba 1,037

katika mashamba ya Serikali; Kununuliwa kwa madume bora 366 ya ng'ombe na kusambazwa kwa wafugaji kupitia vikundi vya wafugaji katika Halmashauri saba (7); Kuzalishwa kwa jumla ya dozi 149,975 za mbegu za mifugo katika Kituo cha Uhimilishaji wa Mifugo (NAIC); na kuhimilisha ng'ombe 124,613 katika mikoa 26.

**f) Uvuvi**

37. Utekelezaji wa miradi katika Sekta ndogo ya Uvuvi iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 135.7 ambapo shilingi bilioni 37.9 zilitolewa sawa na asilimia 27.9. Shughuli na miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa kwa upande wa Sekta ndogo ya Uvuvi ni pamoja na:

i. **Ujenzi wa bandari ya uvuvi na ununuzi wa meli za uvuvi:** Utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko umefikia asilimia 22. Kwa upande wa ununuzi wa meli za uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing), upembuzi wa awali (pre feasibillity study) wa uendeshaji wa meli hizo umekamilika. Aidha, tathmini ya athari za mazingira (Environmental and Social Impact Assessment - ESIA) kwa ajili ya Uvuvi wa Bahari Kuu inaendelea; na

ii. **Upatikanaji wa zana, vifaa na pembejeo za uvuvi na ukuzaji viumbemaji:** Boti 132 zimetengenezwa na kusambazwa; matengenezo ya vizimba 615 vya kufugia samaki yanaendelea; na mafunzo kwa vijana 200 yametolewa na mafunzo kwa vijana wengine 300 wanaojishughulisha na uvuvi na ukuzaji viumbe maji kupitia programu maalum za BBT LIFE (Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora upande wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi) yanaendelea.

**g) Sekta ya Madini**

38. Utekelezaji wa miradi katika Sekta ya Madini uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 22 ambapo shilingi bilioni 12.5 zilitolewa sawa na asilimia 56.9. Shughuli ambazo zimetekelezwa katika Sekta hii ni pamoja na: Ujenzi wa jengo la kuhifadhia sampuli za miamba choronge eneo la Kizota – Dodoma; ununuzi wa magari 12 ya usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za uchimbaji na biashara ya madini nchini; ununuzi wa mitambo mitano (5) ya uchorongaji na mitambo miwili (2) ya kuzalisha mkaa mbadala; utoaji wa leseni 9,640 za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, uyeyushaji na biashara ya madini na utoaji wa leseni mbili (2) za uchimbaji mkubwa wa madini. Aidha, tani 105,985 za makaa ya mawe kati ya tani 276,000 zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2022/23 zilichimbwa na STAMICO katika Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kabulo – Kiwira.

**h) Sekta ya Maji**

39. Utekelezaji wa miradi katika Sekta ya Maji uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 657.9 ambapo shilingi bilioni 619.5 zilitolewa sawa na asilimia 94.2.

Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi ya maji ili kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi waishio vijijini na mijini pamoja na kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini kama ifuatavyo: Kukamilika kwa utekelezaji wa miradi 630 ya vijijini yenye vituo 6,553 vya kuchotea maji hivyo kuwezesha wananchi wapatao 4,393,270 kunufaika na huduma kwenye vijiji 1,390; na kukamilika kwa miradi 67 ya maji na usafi wa mazingira mijini yenye kunufaisha wananchi wapatao 2,566,500. Ukamilishaji wa miradi ya maji vijijini umewezesha wastani wa wananchi wanaopata huduma za maji kuwa asilimia 77 na asilimia 88 kwa mijini kufikia mwezi Juni 2023 ukilinganisha na lengo la asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini itakapofika mwaka 2025. Aidha, kwa upande wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji shughuli zilizofanyika ni kukarabati vituo 136 na kujenga vituo sita (6) vya kufuatilia rasilimali za maji nchini; kukamilisha ukarabati na ujenzi wa mabwawa 11 ya ukubwa wa kati; na kutangaza vyanzo vya maji 41 kuwa maeneo tengefu.

**i) Sekta ya Elimu**

40. Utekelezaji wa programu na miradi katika Sekta ya Elimu uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 2,262.1 ambapo shilingi bilioni 2,538.9 zilitolewa sawa na asilimia 112.2. Serikali iliendelea na utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali katika Sekta ya Elimu kwa kutekeleza programu ya elimu ya awali, Elimumsingi na sekondari ya juu bila ada. Utekelezaji wa programu hizo umewezesha kuandikishwa wanafunzi wapya 1,435,735 wa elimu ya awali; kusajili wanafunzi 1,748,184 wa darasa la kwanza na wanafunzi 784,061 wa kidato cha kwanza. Pia, imewezesha uimarishaji wa miundombinu ya shule kwa kujenga shule 13, madarasa 2,445 ya msingi na sekondari, matundu ya vyoo 6,806 na nyumba za walimu 216; kukamilisha maboma ya madarasa 9,204, mabweni 339, mabwalo 70 na vyumba vya maabara za sayansi 286. Aidha, Serikali imeendelea kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na kuandaa mitaala; pamoja na usambazaji wa nakala 1,687,140 na 4,154,226 za vitabu vya kiada kwa darasa la III – V na darasa la I na II mtawalia na nakala 3,885,000 za vitabu vya ziada kwa ajili ya wanafunzi wa awali. Kwa upande wa rasilimali watu, Serikali imeajiri jumla ya watumishi 13,130 (elimu msingi 7,801 na sekondari 5,329) katika sekta ya elimu.

41. Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya mikoa ya Dodoma (asilimia asilimia 99), Mtwara (asilimia 99), Dar es Salaam (65) na Mwanza (asilimia 64); na kuendelea na ujenzi wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika wilaya 25 (asilimia 98). Aidha, Serikali ilitoa mikopo kwa wanafunzi 198,105; na kutoa udhamini kwa wanafunzi 636 wenye ufaulu wa juu kupitia *Samia Scholarship.*

**j) Sekta ya Afya**

42. Utekelezaji wa programu na miradi katika Sekta ya Afya uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 705.3 ambapo shilingi bilioni 486.8 zilitolewa sawa na

asilimia 69. Serikali ilitekeleza programu na miradi mbalimbali katika Sekta ya Afya iliyolenga kuboresha huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na:

i. **Afya ya msingi:** Serikali imeendelea kuboresha huduma za Afya ya Msingi kwa kujenga na kukamilisha miundombinu pamoja na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba. Mathalan, hospitali 19 za Wilaya zilijengwa na kukamilika, ukarabati wa hospitali kongwe sita (6) umekamilika, ukamilishaji wa zahanati 228 na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya zahanati 288, vituo vya afya 296; na hospitali 69.

ii. **Ngazi ya rufaa:** Shughuli zilizotekelezwa ni: ujenzi na upanuzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa – Muhimbili umefikia asilimia 85, hospitali za Rufaa za Kanda ya Burigi - Chato (asilimia 79) Nyanda za Juu Kusini - Mbeya (asilimia 100), Kanda ya Kusini - Mtwara (asilimia 86), Kanda ya Ziwa - Bugando (asilimia 100), Kanda ya Kati - Benjamin Mkapa (asilimia 24); Kanda ya Kaskazini - KCMC (asilimia 69) pamoja na Hospitali Maalum ya Magonjwa Ambukizi - Kibong'oto, Kilimanjaro (asilimia 84). Aidha, Hospitali 10 za Rufaa za Mikoa zimeendelea kujengwa katika mikoa ya Geita (asilimia 85), Simiyu (asilimia 96), Songwe (asilimia 78), Njombe (asilimia 100), Manyara (asilimia 86), Mawenzi (asilimia 85), Maweni (asilimia 97), Mara (asilimia 69), Morogoro (asilimia 100) na Mbeya (asilimia 98). Vilevile, upatikanaji wa huduma za dawa na chanjo muhimu ulifikia wastani wa asilimia 90. Kwa upande wa watumishi, Serikali imeajiri jumla ya watumishi 8,105 wa kada mbalimbali katika sekta ya afya.

**k) Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara**

43. Utekelezaji wa shughuli na miradi katika Sekta hii uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 30.8 ambapo shilingi bilioni 41.2 zilitolewa sawa na asilimia 133.7. Shughuli na miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa kwa upande wa Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni pamoja na:

i. **Uwekezaji:** Shughuli mbalimbali zilitekelezwa kwa lengo la kuvutia uwekezaji nchini zikiwemo: Kukamilika kwa Sheria ya Uwekezaji Na. 10 ya Mwaka 2022 na Kanuni za Uwekezaji Tanzania za Mwaka 2023; kurekebishwa kwa tozo, ada na faini 106 zinazoweka vikwazo katika mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji; kupatikana kwa hati 601 za mashamba na viwanja zenye ukubwa wa hekta 456,601.254 kwa ajili ya uwekezaji; na kulipa fidia kwa wananchi 1,143 wanaopisha miradi unganishi ya Mchuchuma na Liganga. Aidha, eneo lenye ukubwa wa hekta 78,144.35 linalomilikiwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) limetengwa na kuandaliwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uwekezaji; na

ii. **Viwanda na biashara:** Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: Ukarabati wa viwanda vitatu (3) katika mikoa ya Morogoro, Kilimanjaro na Tanga; ujenzi wa majengo mawili ya viwanda vya SIDO katika mikoa ya Geita (1) na Tanga (1) pamoja na ukarabati wa majengo 12 ya viwanda katika Mikoa sita (6) ya Dar es Salaam (4), Mbeya (1), Arusha (2), Tanga (1) Kigoma (2) na Tabora (2); mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 6.8 imetolewa kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF); na vituo saba (7) vya kuendeleza Teknolojia vimetengeneza jumla ya mashine 714 na vipuri 1,891 vya aina mbalimbali kwa ajili ya viwanda vidogo. Kwa upande wa biashara, TANTRADE imefanikisha upatikanaji wa masoko ya mauzo ya tani 147,061 za mazao zenye thamani ya shilingi bilioni 208.2 yakiwemo mazao ya zabibu, muhogo, mchele, asali, nta na nyama; na kufanyika kwa Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambapo makampuni ya ndani 3,233 na nje 267 kutoka nchi 19 yalishiriki na Mikataba ya kibiashara yenye thamani ya shilingi bilioni 16.98 ilisainiwa.

**l) Sekta ya Utawala Bora**

44. Utekelezaji wa shughuli na miradi katika sekta hii uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 462.7 ambapo shilingi bilioni 472.5 zilitolewa, sawa na asilimia 102.1. Programu na miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa kwa upande wa Sekta ya Utawala Bora ni pamoja na:

i. **Uendelezaji wa mji wa Serikali Mtumba**: Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu na majengo ya ofisi katika Mji wa Serikali – Mtumba. Awamu ya pili ya ujenzi wa ofisi za Wizara 26, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao umefikia wastani wa asilimia 67.8. Ujenzi wa miundombinu ya awali katika Mji wa Serikali - Mtumba ikiwemo maji, umeme, mawasiliano na barabara ambapo mradi wa ujenzi wa barabara (km 51.2) kwa kiwango cha lami umekamilika.

ii. **Ujenzi wa nyumba za viongozi na watumishi**: Serikali ilikamilisha ujenzi wa nyumba 20 za Viongozi Dodoma, ujenzi wa nyumba 150 za watumishi Dodoma (Awamu I) na ukarabati wa Nyumba 40 za Viongozi Dodoma.

iii. **Uboreshaji wa huduma za Mahakama:** Serikali imeendelea kuboresha Huduma za Mahakama ikiwa ni pamoja na**:** kukamilisha ujenzi wa Mahakama za Wilaya 18; Kuendelea na ujenzi wa Jengo la Makao Makuu Jijini Dodoma (asimilia 94); Kujenga na Kukarabati Majengo ya Mahakama za Wilaya sita (6) za Manyoni, Liwale, Kwimba, Ubungo, Korogwe na Ulanga; na nyumba nne (4) za majaji zimejengwa katika

mikoa ya Kilimanjaro, Shinyanga, Mtwara na Tabora. Miradi mingine inayotekelezwa ni ukarabati wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Maswa; na Kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo 10 ambazo ni Mahakama ya Mwanzo Madale - Kinondoni, Kinesi - Rorya, Mahenge - Kilolo, Luilo – Ludewa, Newala – Newala, Usevya – Mlele, Nyakibimbili - Bukoba, Kabanga–Ngara, Mlimba - Kilombero na Mang'ula – Kilombero.

iv. **Ujenzi wa majengo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa:** Serikali imeendelea na ujenzi wa majengo 79 ya utawala ya Halmashauri ambapo majengo ya utawala 10 ya Halmashauri za Wilaya za Mbulu, Momba, Kalambo, Rombo, Mufindi, Iringa, Mafia, Bariadi, Mlele na Halmashauri ya Mji Bariadi umekamilika na majengo mengine yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**m) Sekta ya Ardhi**

45. Utekelezaji wa shughuli na miradi katika Sekta hii uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 101.5 ambapo shilingi bilioni 97.2 zilitolewa sawa na asilimia 95.7. Shughuli na miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa kwa upande wa Sekta ya Ardhi ni pamoja na: Kuandaliwa kwa skimu za uendelezaji maeneo ya mijini kwa majiji ya Mbeya, Mwanza na Arusha; kupimwa kwa viwanja 118,045 kwenye Halmashauri 55; kuandaliwa kwa mipango kina mitano (5) ya uendelezaji upya wa maeneo ya fukwe; Kuimarisha mpaka kati ya Tanzania na Kenya wenye urefu wa kilomita 110 kwa kupima, kuongeza alama, kuboresha zilizoharibika na kuandaa ramani za mipaka; Kuandaliwa kwa mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Halmashauri za wilaya tatu (3) za Nsimbo, Ngorongoro na Kigoma; kuandaa hati za haki ya hatimiliki ya Kimila 7,438 katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete hati 6,594 na Iramba hati 844; na kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi katika Wilaya tano (5) za Maswa, Mbinga, Mafinga, Songwe na Chamwino.

**n) Sekta ya Utalii**

46. Utekelezaji wa shughuli na miradi katika Sekta hii uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 624.1 ambapo shilingi bilioni 613.1 zilitolewa sawa na asilimia 98.2. Serikali imeendelea kuboresha sekta ya utalii ambapo idadi ya watalii imeongezeka hadi kufikia watalii 1,454,920 mwaka 2022 kutoka watalii 922,692 kwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 57.7. Aidha, mapato yaliongezeka kufikia dola za Marekani bilioni 2.5 mwaka 2022 ukilinganisha na dola za Marekani bilioni 1.3 kwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 93. Mafanikio haya yametokana na programu ya Tanzania *The Royal Tour* iliyoasisiwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imetazamwa na watu takribani bilioni 1.2

duniani. Vilevile, Tanzania imetambuliwa na Shirika la *World Economic Forum* (WEF) kuwa ya kwanza katika Bara la Afrika na ya 12 duniani kwa kuwa na vivutio bora vya asili vya utalii na ya 32 kwa Bara la Afrika kwa kuwa na rasilimali bora za malikale.

### 2.4 Fursa Zilizojitokeza katika Utekelezaji wa Bajeti

47. Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23 fursa zilizojitokeza ni pamoja na:

i. Ongezeko la mahitaji ya chakula katika soko la dunia;
ii. Kuongezeka kwa soko la ndani kutokana na ongezeko la idadi ya watu;
iii. Uwepo wa nguvukazi kubwa ya Taifa ambayo ni vijana;
iv. Ukuaji wa miji ambao umekuwa ukifungua fursa nyingi za kiuchumi;
v. Uwepo wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano katika kuwezesha mapinduzi ya nne ya viwanda;
vi. Ufanisi mdogo katika matumizi ya faida ya jiografia ya nchi kuhudumia nchi za EAC, SADC na COMESA;
vii. Uwepo wa amani, umoja na utulivu wa uchumi;
viii. Ongezeko la bei ya vito vya thamani katika soko la dunia;
ix. Uwepo wa vyumba vichache vya kuhudumia watalii ikilinganishwa na ongezeko la idadi ya watalii; na
x. Mahitaji ya viwanda vya ndani kutokana na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi.

48. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujenga uwezo wa ndani wa kutumia rasilimali zilizopo ikiwemo ardhi, misitu, gesi asilia, madini, vyanzo vya maji (bahari, mito na maziwa), nguvu kazi, idadi ya watu, jiografia ya nchi, amani na utulivu na Mkongo wa Taifa ili kuongeza shughuli za uzalishaji bidhaa na huduma.

### 2.5 Changamoto Zilizojitokeza katika Utekelezaji wa Bajeti

49. Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23 changamoto zilizojitokeza ni pamoja na:

i. Kupanda kwa bei ya bidhaa mbalimbali zikiwemo bidhaa za petroli na mbolea kutokana na vita vya Urusi na Ukraine;
ii. Uwepo wa baadhi ya wafanyabiashara wanaokwepa kodi kwa kuingiza bidhaa nchini kwa kupitia njia mbalimbali za udanganyifu zikiwemo magendo;
iii. Mwitikio mdogo wa kutoa na kudai stakabadhi za kielektroniki za EFD wakati wa mauzo;
iv. Ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi; na
v. Upungufu wa fedha za kigeni duniani uliochagizwa na janga la UVIKO-19, vita kati ya Urusi na Ukraine, mabadiliko ya tabianchi na sera za fedha za Marekani, hivyo kuchochea ongezeko la mahitaji ya dola; kuvurugika kwa mfumo wa ugavi, wawekezaji wengi kuwekeza dola zao

Marekani. Athari zilizojitokeza kutokana na upungufu wa fedha za kigeni ni pamoja na kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni la nje na kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa za mtaji na huduma kutoka nje.

### 2.6 Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti

50. Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutatua changamoto zilizojitokeza. Miongoni mwa hatua hizo ni:

i. Kutoa ruzuku kwa ajili ya kupunguza makali ya bei ya bidhaa za petroli kwa kipindi cha Juni hadi Desemba 2022 ;
ii. Kutoa ruzuku kwa ajili ya kupunguza bei ya mbolea na gharama za uzalishaji wa mazao;
iii. Kuendelea kuboresha sheria za kodi, kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato na kuimarisha doria maeneo ya mipakani;
iv. Kutoa elimu kwa walipa kodi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari na matumizi ya stakabadhi za kielektroniki;
v. Kuimarisha usalama wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato;
vi. Benki Kuu kuendelea kusimama sera na Sheria ya Fedha za Kigeni, Sura 271 na Kanuni zake kwa lengo la kudhibiti matumizi holela ya fedha za kigeni; na
vii. Kuingia mikataba mipya kwa kutumia shilingi ya Tanzania kwa lengo la kupunguza uhitaji wa matumizi ya fedha za kigeni yasiyo ya lazima.

### 2.7 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2023/24

**Mapato**

51. Mapato yaliyokusanywa kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2023/24 ni shilingi bilioni 9,163.5. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 6,878.9, sawa na asilimia 95.2 ya lengo la shilingi bilioni 7,224.0. Mapato ya ndani yanajumuisha shilingi bilioni 6,092.2 zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania; shilingi bilioni 491.2 ni mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Idara Zinazojitegemea na Taasisi; na shilingi bilioni 295.4 ni mapato kutoka vyanzo vya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

52. Misaada na mikopo nafuu ilifikia shilingi bilioni 687.5, sawa na asilimia 77.9 ya lengo la shilingi bilioni 882.0. Aidha, mikopo ya kibiashara kutoka masoko ya ndani ilifikia shilingi bilioni 1,220.7, sawa na asilimia 114.2 ya lengo la shilingi bilioni 1,068.7. Mikopo ya kibiashara kutoka nje ilifikia shilingi bilioni 376.4, sawa na asilimia 68.9 ya lengo la shilingi bilioni 546.6. Vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuboresha mifumo ya ukusanyaji, kuanzisha tuzo ya uzalendo wa ulipaji kodi, kuimarisha doria

kwenye maeneo ya mipakani, bahari na maziwa ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa mwaka 2023/24.

**Matumizi**

53. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2023/24, ridhaa ya matumizi ya shilingi bilioni 10,437.7 ilitolewa. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 6,242.1 ni ridhaa ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 4,195.6 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa zinajumuisha: shilingi bilioni 2,446.9 kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni 2,179.8 kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali na matumizi mengine ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali; na shilingi bilioni 1,615.3 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha shilingi bilioni 3,508.1 fedha za ndani na shilingi bilioni 687.5 fedha za nje.

Fedha za matumizi ya maendeleo zilizotolewa zinajumuisha ugharamiaji wa miradi na programu mbalimbali ikiwemo: shilingi bilioni 639.3 kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa; shilingi bilioni 445.9 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara, madaraja na viwanja vya ndege; shilingi bilioni 246.9 kwa ajili ya Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - JNHPP (MW 2,115); shilingi bilioni 114.7 kwa ajili ya miradi ya kilimo; shilingi bilioni 99.9 kwa ajili Programu ya Elimumsingi na Sekondari bila ada; shilingi bilioni 98.1 kwa ajili ya Kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania; shilingi bilioni 92.6 kwa ajili ya mradi wa usambazaji umeme vijijini; na shilingi bilioni 40.7 kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

**Kiambatisho Na. 1C**

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2023/24**

## 3.1 Utangulizi

54. Sehemu hii inaelezea mapitio ya utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2023/24 kwa kuzingatia tathmini na uchambuzi wa bajeti za mafungu kwa mwaka 2023/24 na maoni ya wadau yaliyotolewa katika vikao kazi mbalimbali kuhusu maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

### 3.2 Sura ya Bajeti ya Mwaka 2023/24

55. Kufuatia vipaumbele vya Serikali na maboresho mbalimbali ya kisera na mifumo ya ukusanyaji mapato yaliyofanyika, Sura ya bajeti ya Serikali ilibadilika kutoka mapendekezo ya shilingi bilioni 43,294.6 hadi shilingi bilioni 44,388.1 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 1,093.5 (asilimia 2.5). Kati ya shilingi bilioni 44,388.1 zinazotarajiwa kukusanywa, mapato ya Serikali kuu ni asilimia 68.1, mapato ya Halmashauri asilimia 2.6, misaada na mikopo nafuu asilimia 12.3 na mikopo ya kibiashara ndani na nje asilimia 17.0. Sababu za ongezeko hilo ni kuimarika kwa mwenendo wa makusanyo ya mapato ya ndani pamoja na misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Jedwali Na. 3.1 linaonesha mapendekezo ya Sura ya Bajeti pamoja na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2023/24.

**Jedwali Na. 3.1: Mapendekezo ya Sura ya Bajeti pamoja na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2023/24**

**Shilingi Billioni**

| | Mapato | 2023/24 Baeti Iliyoidhinishwa | 2023/24 Mwongozo | Ongezeko / Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| **A.** | **Mapato ya Ndani-Serikali Kuu** | **30,237.1** | **29,890.7** | **346** |
| | (i) Mapato ya Kodi na yasiyo ya kodi (TRA) | *26,725.4* | *26,379.0* | **346** |
| | (ii) Mapato yasiyo ya kodi | *3,511.7* | *3,511.7* | **0** |
| **B.** | **Mapato ya Halmashauri** | ***1,143.9*** | ***1,143.9*** | **0** |
| **C.** | **Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo** | **5,466.2** | **4,511.0** | **955** |
| | (i) Misaada na Mikopo nafuu - GBS | *2,184.1* | *1,228.9* | **955** |
| | (ii)Misaada na Mikopo nafuu ya Miradi | *3,152.0* | *3,152.0* | **0** |
| | (iii)Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta | *130.1* | *130.1* | **0** |
| **D.** | **Mikopo ya Ndani na Nje** | **7,540.8** | **7,749.1** | **-208** |
| | (i) Mikopo ya Nje | *2,100.5* | *2,110.6* | **-10** |
| | (ii) Mikopo ya Ndani | *1,898.3* | *2,096.4* | **-198** |
| | (iii)Mikopo ya Ndani- Rollover | *3,542.1* | *3,542.1* | **0** |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D)** | **44,388.1** | **43,294.6** | **1,093** |
| | | | | |
| | **Matumizi** | | | |
| **E.** | **Matumizi ya Kawaida** | **30,310.8** | **29,229.0** | **1,082** |
| | (i) Mfuko Mkuu wa Serikali | **12,771.5** | **12,488.2** | **283** |
| | -Malipo ya Riba Ndani | *2,799.4* | *2,736.9* | **63** |
| | -Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover) | *3,542.1* | *3,542.1* | **0** |
| | -Malipo ya Mtaji Nje | *2,763.9* | *2,668.3* | **96** |
| | - Malipo ya Riba Nje | *1,364.4* | *1,239.3* | **125** |
| | - Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii | *1,710.6* | *1,710.6* | **0** |
| | -Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu | *591.2* | *591.2* | **0** |
| | (ii) Mishahara | ***10,882.1*** | ***10,251.3*** | **631** |
| | (iii) Matumizi Mengineyo (OC) | ***5,518.8*** | ***5,527.1*** | **-8** |
| | - Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | *200.0* | *200.0* | **0** |
| | - Matumizi ya Halmashauri (own source) | *689.5* | *697.8* | **-8** |
| | - Matumizi mengineyo | *4,629.4* | *4,629.3* | **0** |
| | (iv) Uhamishaji wa Kawaida wa Maendeleo | *1,138.4* | *962.3* | **176** |
| | -Bodi ya Mikopo | *738.7* | *598.5* | **140** |
| | -Elimumsingi bila Ada | *399.6* | *363.8* | **36** |
| | | | | |
| **F.** | **Matumizi ya Maendeleo** | **14,077.2** | **14,065.7** | **12** |
| | (i) Fedha za Ndani | *10,795.1* | *10,783.6* | **12** |
| | o/w Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | *528.0* | *400.0* | **128** |
| | o/w Ugharamiaji wa SGR | *1,113.0* | *1,500.0* | **-387** |
| | o/w Ugharamiaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere | *1,500.0* | *1,450.0* | **50** |
| | o/w Matumizi ya Halmashauri (own Source) | *454.4* | *394.8* | **60** |
| | o/w Miradi mingine | *7,199.7* | *7,038.8* | **161** |
| | (ii) Fedha za Nje | *3,282.1* | *3,282.1* | **0** |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE (E+F)** | **44,388.1** | **43,294.6** | **1,093** |
| | **NAKISI YA BAJETI (ASILIMIA YA PATO LA TAIFA)** | **2.7%** | **2.7%** | |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

## 3.3 Utekelezaji wa Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2023/24

**a) Uandaaji wa Mpango na Bajeti:** Mafungu yameendelea kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24, sera na miongozo mbalimbali ikiwemo Mpango Mkakati wa Mafungu husika wakati wa maandalizi ya Mipango na Bajeti. Hata hivyo, wakati wa mapitio imebainika ipo

haja ya baadhi ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhuisha Mipango Mikakati ili kuboresha uandaaji wa mipango na bajeti ya mafungu husika.

b) **Utendaji wa Kamati za Bajeti:** Ilibainika kuwa baadhi ya Maafisa Masuuli bado hawajaunda Kamati za Bajeti; Kamati za Bajeti kufanya vikao wakati wa maandalizi ya bajeti peke yake; Mihtasari ya vikao vya kila robo mwaka kutowasilishwa Wizara ya Fedha; baadhi ya Maafisa Masuuli kutoitisha kabisa vikao na kutozingatia muundo sahihi wa wajumbe wanaopaswa kuunda kamati hizo kisheria. Hivyo, ni muhimu Maafisa Masuuli wasisitizwe kuhusu kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti, SURA 439 na kanuni ya 17.

c) **Ukusanyaji wa Mapato:** Mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo yamebaini kuwa, Maafisa Masuuli wameendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa ikiwa ni pamoja na kutumia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG) na kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348. Pia imebainika kuna baadhi ya Taasisi ambazo hazijajiunga na hazitumii mfumo wa GePG. Aidha, imebainika uwepo wa watumishi wasio waadilifu wanaohusika na ukusanyaji wa mapato nje ya Mfumo huo hivyo kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

d) **Kiwango Cha Kubadilishia Fedha:** Wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti Mafungu na Taasisi zilizingatia kiwango elekezi cha ubadilishaji fedha za kigeni cha dola moja ya Marekani kwa Shilingi za Tanzania 2,345.1 kilichobainishwa katika Mwongozo. Hata hivyo, imebainika kuwa baadhi ya Mafungu na Taasisi hazikuzingatia kiwango hicho.

e) **Maandalizi ya Bajeti ya Mishahara na uendeshaji wa Ofisi:** Mafungu yalizingatia miongozo na nyaraka mbalimbali zinazotolewa na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR – MUUUB) na Wizara ya Fedha. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto mbalimbali ikiwemo: kutofautiana kwa taarifa zinazoingizwa kwenye mifumo ya HCMIS na PlanRep/CBMS; kutosomana kwa mifumo mfano HCMIS, GSPP na Mfumo mpya wa Mafao wa PSSSF; na kutokuendana kwa ukomo wa bajeti ya mishahara uliotolewa kwa mwaka 2023/24 na uhalisia wa mahitaji kwa baadhi ya mafungu.

Tathmini ya bajeti ya uendeshaji wa Ofisi ilibaini baadhi ya maeneo kuwa na changamoto katika utekelezaji ikiwemo: kutotengwa kwa bajeti ya kutosha kwa ajili ya kulipa madeni hususan stahiki za watumishi; kutotengwa bajeti kwa ajili ya mafunzo ya watumishi ikiwemo matumizi ya mifumo mbalimbali ya Serikali;

na kutozingatia geresho la kibajeti (GFS Codes 2014) sahihi wakati wa uandaaji wa bajeti.

f) **Maandalizi na Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo** : Mafungu yameendelea kutenga bajeti kwa Miradi ya Maendeleo kulingana na maelekezo yaliyotolewa. Hata hivyo, zipo changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo: Mafungu kuchelewa kufanya malipo kwa wazabuni wanaotekeleza miradi kutokana na changamoto za mifumo; baadhi ya Wizara za Kisekta zinazotekeleza shughuli zinazoshabihiana kutenga bajeti zilizopaswa kutekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na baadhi ya Mafungu kutozingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (Public Investment Management Operational Manual-PIM-OM).

g) **Uzingatiaji Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana:** Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 imeendelea kuzingatiwa. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya ucheleweshaji wa uwasilishaji wa takwimu za miadi ya fedha za nje kwa baadhi ya Mafungu.

h) **Uzingatiaji wa Masuala ya Muungano:** Wizara/Taasisi zimeendelea kuzingatia masuala ya Muungano katika uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 kwa kutenga bajeti ili kuhakikisha vikao vya ushirikiano kati ya Wizara/Taasisi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vinafanyika. Aidha, bajeti kwa ajili ya vikao vya majadiliano ya kupata ufumbuzi wa hoja za Muungano imeendelea kutengwa na taarifa zimeendelea kuwasilishwa Ofisi ya Makamu wa Rais. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya wizara za kisekta kutotenga bajeti ya vikao vya ushirikiano na kupelekea vikao kutofanyika pamoja na kutowasilisha taarifa kuhusu masuala ya Muungano kwa wakati.

i) **Hatua za Kudhibiti Matumizi:** Wakati wa mapitio imebainika kuwa kuna changamoto za utekelezaji zikiwemo: Utaratibu wa baadhi ya watumishi kutumika katika kusimamia miradi inayotekelezwa kwa mfumo wa *Force account* kuathiri utoaji wa huduma hususan afya na elimu; miradi kukosa ubora kutokana na kusimamiwa na watumishi wasio na utaalam katika eneo la ujenzi; baadhi ya mafungu na taasisi kuwasilisha maombi ya fedha bila kuwa na utayari wa matumizi; mafungu na taasisi kuendelea kuzalisha madeni kwa kuingia mikataba na wazabuni nje ya bajeti; baadhi ya mafungu na taasisi kutotenga fedha za kutosha kwa ajili ya mifumo ya udhibiti kama vile ukaguzi wa ndani, ufuatiliaji na tathmini; na upungufu wa watalaam katika kusimamia utekelezaji wa afua mbalimbali ikiwemo miradi ya maendeleo. Aidha, imebainika mafungu na taasisi kutozingatia bei za bidhaa na huduma katika ununuzi ikilinganishwa na bei ya soko na hivyo kuiongezea mzigo Serikali ikizingatiwa kuwa takriban asilimia 60 ya matumizi ya Serikali yanahusu ununuzi.

**j) Utekelezaji wa Masuala Mtambuka:** Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia maelekezo ya kutenga bajeti kwa masuala mtambuka (Kama mapambano dhidi ya rushwa, lishe, UKIMWI, dawa za kulevya, tabianchi na mazingira masuala ya jinsia na makundi yenye mahitaji maalum). Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya mafungu kutenga fedha kidogo za utekelezaji wa masuala mtambuka.

**k) Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa:** Mafungu yameendelea kuwasilisha Hazina makadirio ya michango ya uanachama kwa ajili ya kujumuishwa kwenye Mipango na Bajeti. Hata hivyo, ipo haja ya mafungu kuendelea kuhakikisha makubaliano ya ushirikiano na Taasisi za Kikanda na Kimataifa yanakuwa na manufaa kwa sekta husika na Taifa kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na kushirikisha Wizara ya Fedha na Wizara ya Mambo Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**l) Uzingatiaji wa Maelekezo Mahsusi kwa Taasisi na Mashirika ya Umma:** Serikali imeendelea kufanya maboresho kwenye usimamizi wa Taasisi za Umma ili kuweza kukusanya mapato, kufanya biashara kwa faida na kutoa huduma bora kwa jamii. Hatua zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na kutunga Sheria itakayoanzisha Mamlaka ya Uwekezaji ambayo itaweza kusimamia Mashirika ya Umma na mitaji mikubwa ya Serikali kwenye taasisi ambazo Serikali ina hisa.

Pamoja na mafanikio hayo, zipo changamoto zinazoathiri utendaji wa Mashirika zikiwemo: Baadhi ya Mashirika kuendelea kutegemea ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kinyume na malengo ya kuanzishwa kwake; ukosefu wa mitaji ya kibiashara; na kuingiliana kwa majukumu baina ya taasisi na hivyo kuiongezea gharama Serikali.

**m) Uingizwaji wa Takwimu za Bajeti kwenye Mifumo ya *PlanRep* na *CBMS*:** Mafungu yameendelea kuzingatia uingizaji wa takwimu za bajeti kwenye Mifumo ya *CBMS* na *PlanRep* kwa kuzingatia muda uliopangwa. Hata hivyo, wakati wa mapitio imebainika kuwepo kwa changamoto ya uingizaji wa takwimu zisizo sahihi za bajeti kwenye mifumo ya uandaaji wa bajeti kwa baadhi ya mafungu kutokana na kutofanya mafunzo ya mara kwa mara kuhusu uandaaji wa bajeti na matumizi ya mifumo.

**n) Uwasilishaji wa Randama:** Mafungu yalizingatia ratiba ya uwasilishaji wa Randama. Hata hivyo, imebainika kuwepo kwa utofauti wa muundo (*format*) wa uandaaji wa randama baina ya Mafungu. Hivyo, ni vema kuwepo na muundo (*standardized format*) wa uandaaji wa randama hizo.

**o) Ufuatiliaji, tathimini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa bajeti:** Katika kuimarisha ufuatiliaji na tathmini, Serikali imefanya maboresho ya

kimuundo kwa kuanzisha kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kwa kila Wizara kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa miradi na shughuli mbalimbali za Serikali. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya mafungu kutotenga fedha kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathmini pamoja na upungufu wa watumishi.

p) **Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti:** Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia kwa sehemu maelekezo ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa kuandaa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti za robo mwaka na mwaka mzima. Hata hivyo, tathmini imebaini kuwepo na upungufu wa kujaza baadhi ya fomu kutokana na kutokuwepo kwa mafunzo ya mara kwa mara. Changamoto nyingine ni baadhi ya Mafungu kutoandaa sehemu ya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi na makusanyo na matumizi halisi (Budget Estimate vs Actual Revenue/Expenditure) katika taarifa ya hesabu za mwaka.

q) **Mpangokazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha:** Wizara, Wakala, Idara Zinazojitegemea, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliandaa Mipangokazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha. Hata hivyo, tathmini iliyofanyika imebaini kuwa: Baadhi ya Mafungu hayaingizi takwimu za Mpangokazi na Mtiririko wa Fedha kwa wakati katika Mfumo wa CBMS; taarifa za Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha kutoainisha mahitaji halisi kwa kipindi husika hali inayosababisha kuwepo kwa shughuli zisizotekelezwa kwa kipindi (robo) husika na hivyo kuwepo kwa mrundikano wa shughuli zisizotekelezwa kwa mwaka husika.

r) **Udhibiti wa Vihatarishi:** Maelekezo kuhusu Mipango ya namna ya kukabiliana na Vihatarishi kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa na Kusimamia Mpango wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Taasisi za Umma wa Mwaka 2012 na Kifungu Na. 4 (2) (c) pamoja na Kanuni ya 4 (1) na (2) ya Sheria ya Bajeti, Sura 439, yalilenga kuhakikisha Bajeti inatekelezwa kikamilifu ili kuleta matokeo chanya kwa maendeleo ya Taifa. Hata hivyo, katika utekelezaji wa maelekezo hayo ilibainika kuwa uzingatiwaji ulikuwa si wa kuridhisha kutokana na jitihada za kukabiliana na vihatarishi kutozingatiwa katika Mipango na Bajeti za mafungu husika. Aidha, imebainika baadhi ya mafungu hayana waratibu wa masuala ya vihatarishi, wakuu wa idara na vitengo (risk owners) hawana uelewa wa masuala ya kuainisha vihatarishi, na kutokuhuisha madaftari ya vihatarishi (risk register). Hivyo, upo umuhimu wa kutoa msisitizo ili kuhakikisha masuala ya usimamizi wa vihatarishi yanapewa kipaumbele wakati wa maandalizi ya Mipango na Bajeti pamoja na kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu masuala ya vihatarishi.

s) **Uzingatiaji wa Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa:** Ofisi za Wakuu wa Mikoa zimeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo na

uendeshaji wa ofisi za Mikoa, Wilaya na ofisi za Maafisa Tarafa. Hata hivyo, baadhi ya maelekezo hayakutekelezwa ipasavyo kwa baadhi ya Mikoa na Wilaya yakiwemo: kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka ya Mikoa, Wilaya, Tarafa, na upimaji wa maeneo yanayotegemewa kutekeleza miradi; na kufuatilia uibuaji wa vyanzo vipya na ukusanyaji wa mapato ikiwemo kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kubuni na kuimarisha vyanzo vilivyopo.

**t) Uzingatiaji wa Maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa**

i. **Mgawanyo wa Mapato ya Ndani:** Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetenga jumla ya shilingi bilioni 454.4 kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 35 ya bajeti ya mapato ya ndani kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Uchangiaji wa Miradi ya Maendeleo**

| S/N | Daraja la Halmashauri | Idadi ya Halmashauri | Asilimia ya Kuchangia | Kiasi kilichotengwa (shilingi bilioni) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Daraja la Kwanza | 9 | 70 | 219.85 |
| 2 | Daraja la Pili | 17 | 60 | 77.52 |
| 3 | Daraja la Tatu | 102 | 40 | 138.24 |
| 4 | Daraja la Nne | 56 | 20 | 18.79 |
| | **Jumla** | **184** | **-** | **454.4** |

Aidha, jumla ya shilingi bilioni 8 zimetengwa na Halmashauri 9 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazosimamiwa na TARURA.

Jumla ya shilingi bilioni 87.97 sawa na asilimia 10 ya mapato yasiyolindwa ya shilingi bilioni 879.77 kwa Halmashauri 184 zimetengwa kwa ajili ya utoaji wa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Maelekezo yaliyotolewa kwa Halmashauri kutenga asilimia 20 ya mapato yanayotokana na kilimo hayakuzingatiwa kikamilifu ambapo Halmashauri zilitenga wastani wa asilimia 13.5. Kwa upande wa sekta ya mifugo maelekezo ilikuwa kutenga asilimia 15 ambapo Halmashauri zilitenga wastani wa asilimia 10.4. Aidha, kwa upande wa sekta ya uvuvi Halmashauri zilivuka lengo kwa kutenga asilimia 13.5 ikilinganishwa na lengo la kutenga asilimia 5. Hali hii inaonesha kuwa Halmashauri hazikutenga bajeti za kilimo na mifugo kama ilivyoelekezwa kwa kuzingatia mgawanyo wa asilimia.

ii. **Uzingatiaji wa Maelekezo kuhusu Sekta za Afya, Elimu, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Ardhi, Biashara, Viwanda, Uwekezaji, Maliasili na Mazingira:**

a) Jumla ya Shilingi Bilioni 242.66 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha huduma za afya kwa kutoa kipaumbele katika ununuzi wa dawa, vifaa na vifaa tiba; kujenga, kukamilisha na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya, huduma za mama na mtoto ikiwemo huduma za chanjo; Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu dhana na umuhimu wa bima ya afya ili kufikia lengo la Bima ya Afya kwa Wote;

b) Jumla ya Shilingi bilioni 14.72 zimetengwa kwa watoto 9,400,000 ikiwa zaidi ya Shilingi 1,000 kwa kila mtoto. Aidha, Halmashauri 4 zimetenga chini ya shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano kwa ajili ya huduma za lishe;

c) Takwimu zenye uhalisia kwa ajili ya kuwezesha utengaji wa bajeti ya Elimumsingi na Sekondari (Kidato cha V na VI) ziliandaliwa na kuwezesha utengaji wa bajeti ya elimu bila ada na bajeti ya mishahara ambapo jumla ya shilingi bilioni 676.38 zilitengwa kati ya hizo shilingi bilioni 243.61 ni za mitihani na shilingi bilioni 399.64 za elimu bila ada;

d) Jumla ya Shilingi Bilioni 800.37 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi na sekondari kwa kukamilisha na kukarabati miundombinu ya shule, kutoa nyenzo za kujifunzia na kufundishia hususan vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum; kuwezesha michezo shuleni, kuimarisha masuala ya malezi na makuzi, unasihi, usalama wa mtoto, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni na nyumbani;

e) Jumla ya Halmashauri 16 zimetenga shilingi milioni 353. 27 kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya Ushirika pamoja na kuweka mifumo itakayoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wanaushirika; Kiasi kilichotengwa ni kidogo kulingana na umuhimu wa eneo;

f) Jumla ya shilingi bilioni 22.64 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za biashara, viwanda, maeneo ya uwekezaji na kuendeleza shughuli za wafanyabiashara wadogo;

g) Jumla ya shilingi bilioni 24.32 zilitengwa kwa ajili ya usimamizi na uendelezaji wa maliasili na mazingira ikiwemo: uendelezaji na utangazaji wa vivutio vya utalii, kuhifadhi maeneo oevu, upandaji miti, utunzaji misitu na maeneo ya hifadhi utunzaji wa vyanzo vya maji; na kuhakikisha teknolojia za uzalishaji zinazingatia uhifadhi wa mazingira; uzoaji na uondoshaji wa taka; na

h) Jumla ya Halmashauri 128 kati ya 184 zimetenga bajeti ya shilingi bilioni 23.94 kwa ajili ya kuendeleza na kupanga mipango miji na matumizi bora ya ardhi hususan miji midogo inayochipukia na

kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji, kuendelea na uwekaji wa miundombinu ya anwani za makazi; kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka ya Halmashauri, Kata, Vijiji/Mitaa na Vitongoji na maeneo ya hifadhi. Aidha, upimaji wa maeneo yanayotegemewa kutekelezwa miradi katika halmashauri bado ni changamoto na umepewa kipaumbele kidogo.

**Kiambatisho Na. 1D**

**MUUNDO WA UWASILISHAJI WA MTEF 2024/25 - 2026/27**

**Maelezo ya Kisera kwa Ufupi**

(i) Maelezo ya Waziri/Mkuu wa Mkoa/Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri/Mwenyekiti wa Bodi/Baraza

(ii) Maelezo ya Afisa Masuuli.

**Sura ya 1: Uchambuzi wa Hali Iliyopo**

1.1 Uchambuzi wa Wadau

1.2 Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto

1.3 Masuala Muhimu ikijumuisha mawasilisho ya usimamizi wa vihatarishi

**Sura ya 2: Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti**

2.1 Mapitio ya Utekelezaji - 2022/23

2.1.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2022/23

2.1.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi

2.1.3 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi

2.1.4 Muhtasari wa Malengo yaliyopangwa yakilinganishwa na Malengo yaliyofikiwa

2.2 Mapitio ya Utekelezaji kwa Nusu Mwaka - 2023/24

2.2.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2023/24

2.2.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi

2.2.3 Makadirio ya Matumizi ya Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi

2.2.4 Muhtasari wa Malengo kwenye MTEF yakilinganishwa na Mafanikio yaliyopatikana

2.3 Changamoto zilizojitokeza 2022/23 na Mikakati ya kukabiliana na changamoto

**Sura ya 3: Makadirio ya MTEF (2024/25 - 2026/27)**

3.1 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.1)

3.2 Malengo Makuu, Shabaha na Shughuli zitakazofanyika (Fomu Na. 3A)

3.3 Makadirio ya Matumizi ya Mengineyo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na. 3B)

3.4 Muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida (Fomu Na. 3C)

3.5 Makadirio na Maoteo ya Mapato (Fomu Na.4)

3.6 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.6)

3.7 Muhtasari wa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo (Fomu Na. 6.1)

3.8 Mfumo wa Matokeo wa Kitaasisi (Fomu Na.7)

3.9 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa kila Fungu (Fomu Na. 8A)

3.10 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa Kifungu (Fomu Na. 8B)

3.11 Kipengele Na.I – Muhtasari wa Wafanyakazi Walio kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara (Fomu Na. 8C)

3.12 Kipengele Na.II - Muhtasari wa Watumishi Wenye Kibali Wanaotarajiwa Kuajiriwa Katika Mwaka husika (Fomu Na. 8D)

3.13 Kipengele Na.III - Muhtasari wa Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kuajiriwa (Fomu Na. 8E)

3.14 Orodha ya Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kustaafu (Fomu Na. 8F)

3.15 Jedwali la Mishahara kulingana na Ikama (Fomu Na. 9)

3.16 Fomu ya Taarifa za Miradi (Fomu Na. 10A)

3.17 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Miradi kwa mwaka unaofuata kwa Fungu (Fomu Na. 10C)

**Kiambatisho Na. 1E**

**RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**JINA LA FUNGU ..........................**

**FUNGU NA .........**

**RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25**

**Imetayarishwa na;**

Anuani ya Fungu

**Machi,** 2024

**YALIYOMO**

**VIFUPISHO**

**SURA YA KWANZA**

**1. UTANGULIZI**

- 1.1. Dira
- 1.2. Dhima
- 1.3. Majukumu ya Fungu

**SURA YA PILI**

**2. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA FUNGU YA MWAKA 2023/24**

- 2.1. Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati…
- 2.2. Tathmini ya Utekelezaji Bajeti hadi Februari 2024
  - 2.2.1. Taarifa ya Fedha Zilizovuka Mwaka 2022/23 (**Jedwali Na. 1**)
  - 2.2.2. Mapato/Maduhuli (**Jedwali Na. 2**)
  - 2.2.3. Matumizi ya Kawaida
  - 2.2.4. Miradi ya Maendeleo
- 2.3. Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti
- 2.4. Changamoto (kama zipo) ambazo ni muhimu Kamati ya Bunge ikazifahamu na Mikakati ya Kuboresha Utekelezaji wa Bajeti

**SURA YA TATU**

**3. MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2024/25**

- 3.1. Vipaumbele vya Mpango na Bajeti
- 3.2. Makadirio ya Mapato
- 3.3. Makadirio ya Matumizi ya kawaida
  - 3.3.1. Kazi zitakazotekelezwa (kifungu kwa kifungu) (**Jedwali Na. 3**)
- 3.4. Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo
  - 3.4.1. Miradi Itakayotekelezwa (**Jedwali Na. 4**)
- 3.5. Muhtasari wa Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2024/25 (**Jedwali Na.5**)

  *Muhtasari uoneshe maombi ya fedha kwa Fungu husika na mchanganuo wake*

**Jedwali Na. 1: Taarifa ya Fedha Zilizovuka Mwaka ….**

| Geresho la Mradi | Jina la Mradi | Shughuli zilizoombewa Kibali | Fedha zilizovuka Mwaka 2022/23 | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha zilizobaki Kufikia Juni, 2022 | Fedha zilizotumika hadi Feb 2024 | Kazi zilizotekelezwa |
| 5401 | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya | | 68,213,114 | 45,490,000 | Fedha zimetumika kukamilisha shughuli za kuweka tiles, kupaka rangi, kuweka milango na madirisha, |

**Jedwali Na. 2**: **Tathmini ya Ukusanyaji Mapato ya Ndani / Maduhuli**

| Mapato Yaliyoidhinishwa | Makusanyo Halisi | Ufanisi (Asilimia) | Sababu za Ufanisi |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida Mwaka …**

**Geresho la Kifungu:** Mfano 1001
**Jina la Kifungu:** Mfano Utawala na Rasilimali Watu

| NA. | KASMA | MAELEZO YA KASMA | KIASI KILICHOTENGWA | | MAELEZO YA MATUMIZI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2023/24 | 2024/25 | |
| 1. | 21111 | Mishahara ya watumishi | 50,000,000 | 60,000,000 | Kitengo kinaomba kuidhinishiwa **shilingi 600,000,000** kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi 30 walio katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni.<br>Kasma hii imeongezeka kwa **shilingi 100,000,000** kutokana ongezeko la watumishi watatu |

| NA. | KASMA | MAELEZO YA KASMA | KIASI KILICHOTENGWA | | MAELEZO YA MATUMIZI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2023/24 | 2024/25 | |
| | | | | | (3) katika kitengo. |

**Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Maendeleo Mwaka …**

**Geresho la Kifungu:** Mfano 1001

**Jina la Kifungu:** Mfano Utawala na Rasilimali Watu

| Geresho la Mradi | Jina la Mradi | Shughuli zilizopangwa kutekelezwa | Gharama za Mradi | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za ndani | Fedha za nje |
| 4321: | Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (Primary Education Development Programme) | Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) Awamu ya Pili – GPE LANES II | - | 2,000,000 |

**Jedwali Na. 5: Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka….**

| Maelezo | | | Bajeti 2024/25 |
|---|---|---|---|
| 1 | Matumizi ya Kawaida | Mishahara | |
| | | Matumizi Mengineyo | |
| | **Jumla Ndogo** | | |
| 2 | Matumizi ya Maendeleo | Ndani | |
| | | Nje | |
| | **Jumla Ndogo** | | |
| **Jumla Kuu** | | | |

**Kiambatisho Na. 1F**

## MUUNDO WA TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI

Ukurasa wa juu
Yaliyomo
Vifupisho vya maneno

Utangulizi

Sehemu hii itahusisha maelezo mafupi juu ya wajibu na majukumu ya Kamati katika usimamizi wa bajeti; orodha ya wajumbe na kumbukumbu za barua za uteuzi kwa mujibu wa sheria ya bajeti na orodha ya agenda zilizojadiliwa

1.0 Uendeshaji wa vikao

Sehemu hii itahusisha Ratiba na utaratibu wa uendeshaji wa vikao

2.0 Mapitio ya Muhtasari wa kikao cha kamati kilichopita

Elezea kwa ufupi maazimio ya kikao kilichopita

3.0 Ugawaji wa Rasilimali:

- 3.1 Mgawanyo wa rasilimali kulingana na vipaumbele vya bajeti kama ilivyoainishwa kwenye mpango kazi
- 3.2 Utaratibu wa ugawaji wa rasilimali kila mwezi kulingana na vipaumbele vya bajeti
- 3.3 Mgawanyo wa rasilimali fedha katika Idara na Vitengo

4.0 Taarifa ya kazi zilizotekelezwa nje ya mpango na bajeti

5.0 Mafanikio, Changamoto na Mapendekezo

6.0 Hitimisho

Wizara ya Fedha
Treasury Square Building 18
Jakaya Kikwete Road
S.L.P 2802, 40468 Dodoma.
Barua pepe:
info@hazina.go.tz
Simu: +255 26 2160000